# KUCHUNGUZA UBIBLIA KATIKA TAMTHILIYA ZA EMMANUEL MBOGO

**EMMANUEL OSCAR MSANGI**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2018**

# ITHIBATI

Aliyeweka saini hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma tasnifu hii iitwayo: "**Kuchunguza Ubiblia Katika Tamthiliya za Emmanuel Mbogo"** na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya Shahada ya Uzamili (MA) katika Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

………………………………..

**Dkt. Mohamed Omari Maguo**

(Msimamizi)

…….………………………

**Tarehe**

## HAKIMILIKI

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa njia yoyote ile, iwe kazi nzima au sehemu ya kazi hii bila kibali cha maandishi cha Mkuu wa Kurugenzi ya Taaluma za Uzamili na Uzamivu, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, kwa niaba ya mwandishi, isipokuwa kwa shughuli halali, kama vile kwa ajili ya utafiti, kujisomea au kufanya marejeo ya kitaaluma.

## TAMKO

Mimi **Emmanuel Oscar Msangi,** nathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu halisi na kwamba haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya masharti ya kupata shahada kama hii au nyingine yoyote.

…………………..………………

**Sahihi**

……………………………

**Tarehe**

# TABARUKU

Kazi hii ninaitabaruku kwa bibi yangu mpenzi, Emmy Eliezer Taluka kwa malezi bora na upendo mkuu mkuu aliouonyesha kwangu siku zote za maisha yake. Sala na duwa zake zimenijaalia kukamilisha kazi hii. Naitabaruku kwake iwe kumbukumbu yake kwa vizazi vingine vingi vijavyo.

## SHUKURANI

Kwa heshima kubwa, ninamshukuru Mungu muweza wa yote kwa kunijalia uzima na afya, ulinzi na maarifa wakati wote wa masomo yangu ya uzamili. Wakati wote wa masomo yangu amekuwa nami. Ameniongoza, amenishika kwa mkono wake na kunipa kibali pote nilipoingia na kutoka kipindi chote cha masomo yangu.

**Pili**, napenda kumshukuru kwa dhati msimamizi wangu Dkt. Mohammed Omar Maguo kwa kuniongoza vema katika kila hatua ya utafiti huu. Hakusita wala hakuchoka kunishauri na kuirekebisha kazi hii katika hatua zote mpaka ilipokamilika. Amenilea kitaaluma na kunipa misingi ya nadharia za fasihi, mwingilianomatini na mbinu za utafiti ambazo zimesaidia kukamilika kwa kazi hii. Namuomba Mungu ambariki na ampe afya njema na amzidishie kila la kheri katika huduma yake hii ya ukufunzi na usimamizi wa tafiti. Amin!

**Tatu**, natoa shukrani zangu za dhati kwa Mkuu wangu wa Idara; Dkt Zelda Elisifa, Idara ya Taaluma za Isimu na Fasihi, hapa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania chini ya Idara ya Taaluma za Isimu na Fasihi, Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii kwa kukubali kunidhamini katika masomo yangu. Ninasema asante sana!

**Nne**, Ninawashukuru walimu wangu wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa kunilea kitaaluma na kunikuza kinadharia na vitendo. Walimu hao ni Profesa Emmanuel Mbogo, Profesa Tigiti Sengo, Dkt Hilda Pembe, Dkt Hadija Jilala, Dkt Hanna Simpassa, Dkt Nestory Ligembe, Mwl Bakari Kombo na Dkt Dunlop Ochieng.

**Tano**, ninawashukuru sana wazazi wangu, Oscar Emmanuel na Kalitas Maembe. Wazazi hawa wamenilea, kunitunza na kunipeleka shule katika ngazi mbalimbali hadi hapa nilipofikia. Baba na Mama, ninawashukuru sana! Kijana wenu ninawapenda na kuwathamini mno!

Mwisho (si kwa umuhimu), ninawashukuru Dkt Emmanuel Lema wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Mwalimu Herman Bakize wa Chuo Kikuu cha Zimbabwe kwa ushauri wao nilipowafuata wakati wa utafiti na wengine wote ambao wameshiriki kwa namna mbalimbali kusaidia utafiti na uandishi wa tasnifu hii kukamilika. Mungu awabariki wote walioshiriki kwa namna moja ama nyingine.

Nyote pamoja, asanteni sana!

# IKISIRI

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuchunguza ubiblia katika tamthiliya za Emmanuel Mbogo kupitia tamthiliya zake za *Nyerere na Safari ya Kanaani* (2015) na *Sadaka ya John Okello* (2015). Ili kufikia lengo kuu tulikuwa na malengo mahsusi mawili; kubainisha utokezaji wa Ubiblia katika tamthiliya za Emmanuel Mbogo na kueleza sababu za utokezaji wa Biblia/mwangwi wa Biblia katika kazi hizo teule za Emmanuel Mbogo. Sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa. Tamthiliya teule za *Sadaka ya John Okello* na *Nyerere na Safari ya Kanaani*, ziliteulewa kwa maksudi kabisa kwa kuwa ndizo ambazo zimeweza kumpatia mtafiti data alizozihitaji. Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini. Uchambuzi wa data katika utafiti huu ulifanywa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo. Aidha ukusanyaji, uchambuzi na kujadili data kuliongozwa na nadharia ya mwingilianomatini. Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa kuna Ubiblia mwingi katika tamthiliya za Emmanuel Mbogo alizoziandika miaka ya karibuni. Vipengele vya kifani ndivyo vimetumika katika kubainisha ubiblia huo. Vipengele hivyo ni jina la kitabu, hadithi za kibiblia, wahusika wa kibiblia, nukuu za kibiblia na mtindo wa ushairi. Tamthiliya hizi mbili tulizozitafiti za Emmanuel Mbogo; *Sadaka ya John Okello* na *Nyerere na Safari ya Kanaani* zimeakisi mwangwi mkubwa wa Biblia. Kwa mfano kisakale cha wana wa Israel kukaa utumwani Misri na kisha kuanza safari kurejea kwao Kanaani katika Biblia kinapatikana kitabu cha “Kutoka”. Kisakale hiki kimeakisiwa kwa wingi katika tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani*, Kanaani ni nchi iliyojaa maziwa na asali kwa mujibu wa kisakale hicho.

# YALIYOMO

**ITHIBATI** .......... **ii**

**HAKIMILIKI** .......... **iii**

**TAMKO** .......... **iv**

**TABARUKU** .......... **v**

**SHUKURANI** .......... **vi**

**IKISIRI** .......... **viii**

**SURA YA KWANZA** .......... **1**

**1.0 UTANGULIZI KWA JUMLA** .......... **1**

1.1 Utangulizi .......... 1

1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti .......... 1

1.4.1 Malengo Mahsusi ya Utafiti .......... 7

1.4.2 Maswali ya Utafiti .......... 7

1.5 Umuhimu wa Utafiti .......... 7

1.6 Mipaka ya Utafiti .......... 9

1.7 Mpangilio wa Tasnifu .......... 10

**SURA YA PILI** .......... **11**

**2.0 UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA** .......... **11**

2.1 Utangulizi kwa Jumla .......... 11

2.2 Maana ya Tamthiliya na Sifa zake .......... 11

2.3 Mwingilianomatini katika Tamthiliya za Kiswahili .......... 16

2.4 Wasifu wa Emmanuel Mbogo .......... 19

2.5 Muhtasari wa Tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani* .......... 23

2.6 Muhtasari wa Tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* ........ 25

2.7 Kazi Tangulizi Kuhusu Tamthiliya za Emmanuel Mbogo ........ 27

2.8 Pengo la Maarifa ........ 30

2.9 Mkabala wa Kinadharia ........ 30

2.9.1 Nadharia ya Mwingilianomatini ........ 31

2.10 Hitimisho ........ 35

**SURA YA TATU ........ 36**

**3.0 MBINU ZA UTAFITI ........ 36**

3.1 Utangulizi ........ 36

3.2 Eneo la Utafiti ........ 36

3.3 Usanifu wa Utafiti ........ 37

3.4 Sampuli na Usampulishaji ........ 37

3.5 Aina ya Data zilizokusanywa ........ 38

3.5.1 Data za Msingi ........ 39

3.5.2 Data za Upili ........ 39

3.6 Mbinu za Kukusanya Data ........ 39

3.6.1 Usomaji Makini ........ 40

3.7 Mbinu ya Uchambuzi wa Data ........ 41

3.7.1 Mkabala wa Kimaelezo ........ 41

3.8 Usahihi na Kuaminika kwa Data ........ 42

3.9 Maadili ya Utafiti ........ 42

3.10 Hitimisho ........ 42

**SURA YA NNE ........ 44**

**4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ZA UTAFITI ........ 44**

4.1 Utangulizi ... 44

4.2 Ubiblia na Sababu za Utokezaji wake katika *Nyerere na Safari* ... 44

4.2.1 Jina la Kitabu ... 45

4.2.2 Hadithi ya Biblia ... 50

4.2.3 Wahusika wa Biblia ... 57

4.2.4 Nukuu za Biblia ... 63

4.2.5 Matumizi ya Ushairi/Zaburi ... 68

4.3 Hitimisho ... 72

**SURA YA TANO ... 73**

**5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ... 73**

5.1 Utangulizi ... 73

5.2 Muhtasari ... 73

5.3 Hitimisho ... 77

5.4 Mapendekezo ... 78

**MAREJELEO ... 79**

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI KWA JUMLA

### 1.1 Utangulizi

Katika sura hii tumebainisha tatizo la utafiti lililofanyiwa uchunguzi katika utafiti tulioufanya. Sura hii inabanisha na kueleza usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, mipaka ya utafiti, maswali ya utafiti ambayo utafiti huu ulikusudia kuyajibu pamoja na umuhimu wa utafiti huu. Kimsingi tunaweka bayana hapa kuwa katika utafiti huu dhana ya ubiblia itachukuliwa kwa maana ya vipengele vyote vilivyomo ama vilivyotumika kwenye kazi ya fasihi, tamthiliya vyenye mwangwi wa kibiblia. Vipengele hivyo vinaweza kuwa majina ya vitabu, majina ya wahusika na uhusika wao, hadithi za kibiblia, mashairi ya kibiblia, nukuu za kibiblia n.k.

### 1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Ubiblia katika kazi za fasihi si dhana ngeni. Mtindo huu umeshajitokeza katika kazi mbalimbali za fasihi andishi; riwaya, tamthiliya na ushairi. Waandishi na watafiti mbalimbali wamekwisha uchunguza na kuuandikia. Hapa Afrika baadhi ya watunzi wameutumia mtindo huu katika uumbaji wa kazi zao. Kwa mfano Ngugi wa Thiong'o katika kazi zake za *A Grain of Wheat* (1967) na *The Devil on the Cross/Shetani Msalabani* (1982). Kazi hizi zina mwangwi wa Biblia ndani yake. Jacob Mapara (2003) kutoka huko Zimbabwe alitalii kuhusu Biblia na fasihi katika tasnifu yake ya uzamili aliyoipa jina, "The Bible and Literature: A case study in some Shona novels." Utafiti ulifanyika huko Zimbabwe katika fasihi ya Kishona. Katika fasihi ya Kiswahili, Mtunzi Euphrase Kezilahabi naye aliutumia mtindo huu

hasa katika riwaya yake iitwayo *Rosa Mistika*. Hata hivyo watafiti wameonekana kuugusa zaidi utanzu wa riwaya katika tafiti zao walipochunguza mwingiliano wa Biblia na fasihi na kusahau upande wa tamthiliya ambao ndiyo utashughulikiwa katika utafiti huu. Kwa sababu tutajikita zaidi kwenye kutazama mwingiano wa fasihi na Biblia ni vema tutazame kwanza dhana ya mwingilianomatini inavyojadiliwa kutoka vyanzo mbalimbali vya maarifa.

Dhana ya mwingilianomatini ni miongoni mwa nadharia za fasihi, ambayo hutumika kuchunguza, kuchambua data za utafiti na kubaini kazi moja ndani ya kazi nyingine katika kazi za fasihi. Dhana hii hutumika pia kuelezea kuwepo kwa sifa mbalimbali za matini moja au zaidi katika kazi za fasihi. Pia dhana hii ya mwingilianomatini hurejelea uhusiano uliopo kati ya matini husika na nyingine ambazo msomaji au mwandishi amewahi kukutana nazo kabla ya hiyo iliyoko mbele yake wakati huo.

Plotell na Charney (1978) wanaeleza kuwa, dhana ya mwingilianomatini inarejelea msingi kuwa matini ya kisanaa si zao la mwandishi mmoja bali ni zao la jinsi matini hiyo inavyohusiana na matini nyingine na umbo la lugha yenyewe. Dhana hii husisitiza kwamba, matini zote za kisanaa zaweza kuchukuliwa kama matini moja kuu ambapo hujibizana, kila moja ikisemezana na nyingine kwenye usemezano uliotanuliwa. Kimsingi dhana hii ya mwingilianomatini inahusishwa na mnadharia wa Kifaransa, Julia Kristeva ambaye aliizua kutokana na nadharia ya Mikhail Bakhtin ya Usemezano. Usemezano hutumiwa kuelezea kuwepo kwa sifa mbalimbali za matini moja au zaidi katika kazi za fasihi. Uhusiano huu unaozungumzwa unaweza kuonekana katika nukuu yaani matini fulani kuwa na nukuu ya matini nyingine ambayo ilianza kwanza, uelezwaji wa jambo moja kwa

moja au kutumia lugha zinazofanana. Katika fasihi ya Kiswahili tafiti nyingi zimekwishafanyika kuhusu mwingilianomatini unaojitokeza katika kazi mbalimbali katika uga huu wa kisanaa. Kuna watafiti waliotazama mwingilianomatini katika riwaya, wengine tamthiliya na wengine ushairi.

Utafiti huu unachunguza mwingilianomatini wa Biblia na fasihi katika kazi teule za Emmanuel Mbogo (*Nyerere na Safari ya Kanaani* na *Sadaka ya John Okello*). Tunachunguza namna mwangwi wa Biblia unavyojitokeza katika kazi za mwandishi huyu nguli katika fasihi ya Kiswahili, mbobevu kwenye uga wa sanaa za maonyesho na filamu nchini Tanzania. Kazi kadhaa alizoandika mwandishi huyu, zimetawaliwa na mwingiliano mkubwa baina ya Biblia na fasihi. Mtu asomapo kazi hizo kuna mwangwi mkubwa wa Biblia unaoonekana akilini mwake, kukumbuka au kuona kitushi fulani moja kwa moja kilichomo kwenye Biblia.

Mtafiti mwingine anayeitwa Mapara (2003), katika tasnifu yake ya *The Bible and Literature: A Case Study in some Shona Novels*. Anaeleza kwamba usomaji na uhakiki wa kazi za fasihi ni zoezi endelevu hapa ulimwenguni. Nadharia mbalimbali zinazotumika kusoma na kuhakiki kazi hizi za fasihi zimempa msomaji wake macho mapana yanayomwezesha kuyaona waziwazi yale yaliyomo ndani ya kazi ya fasihi husika. Nadharia kama ufeministi, umuundoleo, ubunilizi, umapinduzi (tukitaja chache) zimefungua sana macho ya msomaji. Mapara (amekwishatajwa) anaendelea kusema kwamba, katika muktadha wa kijamii ni vema kung'amua kwamba, saikolojia ya mtu inanolewa na kutawaliwa na mazingira aliyomo. Mazingira mwandishi aliyomo ndiyo huchochea mwandishi au mtunzi kuandika chochote kwa ajili ya hadhira yake, japo si lazima aandike kile hadhira yake inakihitaji. Laweza

kuwa jambo linalojulikana na hadhira au la! Vilevile mwanazuoni Webb (1980:24) anasema kwamba, "*Each work of art arises out of the particular of its time*." Kwamba, kila kazi ya sanaa ni tokeo la wakati fulani maalum ama muhula wake mahsusi. Dai hili linatutazamisha kuwa Emmanuel Mbogo amekusudia kutoa ujumbe kwa hadhira yake kwa kutumia taswira na jumbe za Biblia tofauti na kazi zake za awali.

Emmanuel Mbogo ametumia kazi zake kuhubiri! Ndiyo! Kuna nadharia kwamba, Mwanafasihi ni kama muhubiri mimbarini. Tunahofu kuwa watu wengine huenda wasielewe mtindo huu. Utafiti umetazama chanzo cha kazi husika na uhakiki wake. Utafiti unakusudia kuonyesha kuwa Biblia imetumika kama chanzo (kichocheo) kwa mwandishi katika kuzaa kazi hizo husika za fasihi.

Hapa Afrika waandishi wengine wamekwisha utumia mtindo huu. Kwa mfano Ngugi wa Thiong'o katika kazi zake za *A Grain of Wheat* na *The Devil on the Cross/Shetani Msalabani*. Tutazungumza zaidi huko mbele kuhusu mtunzi huyu na kazi zake mbalimbali zenye harufu ya Biblia ndani yake. Kezilahabi naye aliutumia mtindo huu hasa katika kazi yake ya *Rosa Mistika*. Waandishi wanaotumia mtindo huu, ubiblia huweza kudhihirika kupitia majina ya wahusika wao, majina ya kazi zao, mf: *The Devil on The Cross* (Ngugi) na *Nyerere na Safari ya Kanaani* (Mbogo), dhamira zake n.k Wanazuoni wengine waliotazama dhana hii ya mwingilianomatini katika tamthiliya ni Ambrose na wenzake (2015). Wao walitafiti na kutazama mwingilianomatini katika tamthiliya za Kiswahili. Makala yao waliipa jina, *"*Mwingilianomatini katika Tamthiliya za Kiswahili: Mashetani na Kijiba cha Moyo*"*. Makala haya yalichunguza viwango na aina za mwingilianomatini baina ya

tamthiliya mbili za Kiswahili. Tamthiliya hizo zilikuwa *Mashetani* (Ebrahim Hussein 1971) na *Kijiba cha Moyo* (Arege Timothy 2009). Katika makala haya waandishi wametazama namna tamthiliya hizi mbili zinavyofanana kwa kutumia vipengele vya motifu, maudhui, matumizi ya lugha na wahusika. Wametazama kwa kiasi gani utunzi wa *Kijiba cha Moyo* umeathiriwa na mtunzi wa *Mashetani*. Tamthiliya ya *Mashetani* kiwakati (1971), ndiyo iliyotangulia kuzaliwa na kutungwa. Kwa hivyo waling'amua kuwa Timothy Arege kabla ya kuitunga kazi yake hiyo ya *Kijiba cha Moyo* (2009) alishakutana na kazi ya *Mashetani* na kwa hivyo ikamuathiri katika utunzi wake.

Mningo (2015) katika tasnifu yake ya uzamili, "Tathimini ya Mwingilianomatini katika Utunzi wa Emmanuel Mbogo: Utafiti Linganishi wa Tamthiliya ya Ngoma ya Ng'wanamalundi na Fumo Liyongo*."* Lengo kuu la utafiti huo lilikuwa ni kufanya tathmini ya mwingilianomatini katika utunzi wa Emmanuel Mbogo, kwa kulinganisha tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1988) na *Fumo Liongo* (2009), ili kubaini jinsi mtunzi huyo anavyofumbata mbinu ya mwingilianomatini katika kazi zake za fasihi, na namna mbinu hiyo inavyotumika kuibua dhamira za tamthiliya hizo. Katika sehemu hii tumeona kwamba dhana ya mwingilianomatini imeshawashughulisha wanazuoni na watafiti kutoka pahala pengi isomwapo na kufundishwa fasihi ya Kiswahili.

Pengine mada lengwa ndiyo inayoweza kuleta upya au kuzungumzia kitu kipya ambacho watafiti bado hawajakizungumza katika tafiti zao. Kimsingi katika tasnifu hii tumebainisha ubiblia ulivyojitokeza katika kazi teule za Emmanuel Mbogo.

Sambamba na hilo tumeeleza sababu za kujitokeza kwa ubiblia katika kazi hizo; tamthiliya za *Nyerere na Safari ya Kanaani* na *Sadaka ya John Okello*.

### 1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti

Watafiti katika fasihi ya Kiswahili wamesoma na kuhakiki kazi mbalimbali za mwandishi Emmanuel Mbogo. Mathalani, Clemence (2015) amechunguza mbinu za kibunilizi katika tamthiliya za Sundiata na Fumo Liyongo. Kimambo (2015) ametafiti kuhusu matumizi ya lugha katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha* na Msacky (2014) ametafiti usawiri wa nafasi ya mwanamke katika tamthiliya ya *Watoto wa Mama Ntilie*, tukitaja wachache. Hata hivyo, watafiti waliotangulia kutafiti kuhusu Emmanuel Mbogo, hawajawahi kufanya utafiti kuhusu mada lengwa tuliyoifanyia utafiti. Kutotafiti mada hii hapo kwanza kumetengeneza pengo la maarifa katika fasihi na uga wa sanaa kwa jumla ambalo utafiti huu umeliziba.

Tamthilia hizi, *Nyerere na Safari ya Kanaani* na *Sadaka ya John Okello* hazijawahi kufanyiwa utafiti kwa mwelekeo huu wa kuchunguza ubiblia kati yazo. Kwa maoni yetu inafaa kuitumia nadharia hii ya mwingilianomatini katika kuhakiki tamthilia za Kiswahili ili kuchangia katika kuziba pengo hili ambalo watafiti wengine hawajalishughulikia. Utafiti utaonyesha ubiblia uliomo katika tamthiliya za Emmanuel Mbogo na kueleza sababu za utokezaji wake katika tamthiliya hizo. Hili tunalolitafiti halijapata kushughulikiwa hapo kwanza na wanazuoni wengi waliowahi kutafiti kazi za mwandishi huyu gwiji katika tamthiliya ya Kiswahili. Tulipotalii tafiti zinazohusu uhakiki wa fasihi, nadharia ya mwingilianomatini haijatumiwa sana

katika uchanganuzi wa fasihi ya Kiswahili. Hii ni kinyume na nadharia nyingine ambazo zimetumika na zimechangiwa na wataalamu wengi. Ni kutokana na jambo hili tumefikiri kuwa kuna umuhimu wa kuitumia ili kuonyesha utendakazi wake katika uhakiki wa fasihi ya Kiswahili.

## 1.4 Lengo Kuu

Kuchunguza Ubiblia katika Tamthiliya za Emmanuel Mbogo kupitia tamthiliya zake za *Sadaka ya John Okello* (2015) na *Nyerere na Safari ya Kanaani* (2015).

### 1.4.1 Malengo Mahsusi ya Utafiti

i. Kubainisha vipengele vya wa kibiblia vinavyojitokeza katika tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo; *Nyerere na Safari ya Kanaani* na *Sadaka ya John Okello*.

ii. Kueleza sababu za ujitokezaji wa vipengele vya kibiblia katika tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo; *Nyerere na Safari ya Kanaani* na *Sadaka ya John Okello.*

### 1.4.2 Maswali ya Utafiti

i. Vipengele vya kibiblia vinajitokezaje katika tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo; *Nyerere na Safari ya Kanaani* na *Sadaka ya John Okello*?

ii. Kwa nini vipengele vya kibiblia vinajitokeza katika tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo; *Nyerere na Safari ya Kanaani* na *Sadaka ya John Okello*?

## 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utakuwa umuhimu katika nyanja za kinadharia, kitaaluma na kitamaduni. Kinadharia, utafiti huu utatoa mchango mkubwa katika kuielewa nadharia ya mwingilianomatini na jinsi inavyojitokeza katika utunzi wa kazi za fasihi na uhakiki pia. Watafiti wataelewa kwamba Emmanuel Mbogo aliongozwa na nadharia ya

mwingilianomatini katika utunzi wa tamthiliya zake ambazo zimejumuisha sifa za ubiblia ndani yake. Watafiti watabaini kuwa nadharia za kifasihi zinaweza kuwa msingi wa utunzi wa kazi fulani mahsusi za wasanii na si kutumika kufanya uhakiki tu kama ilivyo kaida ya watafiti na wahakiki wengi wa kazi za fasihi. Katika uga wa taaluma, utafiti huu tulioufanya utakuwa ni rejeleo muhimu kwa wanazuoni wanaotalii fasihi ya Kiswahili, haswa uga wa tamthiliya pamoja na masuala ya nadharia na uhakiki wa kazi za fasihi.

Utafiti huu ulikusudiwa kuwa wa kwanza au kuwa miongoni mwa kazi chache zilizojadili kuhusu mada husika katika fasihi ya Kiswahili. Utawafaa wanazuoni katika uga wa fasihi kwa jumla. Hazina kubwa ya maarifa kuhusu mwingilianomatini wa Biblia na fasihi iliyoibuliwa katika utafiti huu kwa kuchunguza ubiblia ulivyojitokeza katika kazi hizi itakuwa rejea nzuri kabisa kwa watafiti wajao watakaotaka kuchunguza mwingilianomatini katika kazi nyingine za Emmanuel Mbogo na watunzi wengine katika fasihi ya Kiswahili. Kazi hii itakuwa dira njema kwa wanazuoni wote wa fasihi wasomapo ama kuzungumza kuhusu mwingilianomatini katika kazi za Emmanuel Mbogo.

Kwa upande wa utamaduni, utafiti huu utatoa mchango mkubwa kuvielewa vema vitushi mbalimbali vilivyotumiwa kujenga tamthiliya hizi kutoka katika Biblia. Dini ni kipengele mojawapo cha utamaduni. Emmanuel Mbogo ni Mkristo kwa kuzaliwa, amekulia na kuzeekea Ukristo hivyo si ajabu kuona kwamba imani hiyo anayoiamini ikijitokeza katika kazi zake. Wahenga wanasema, kimjazacho mtu ndicho kimtokacho. Kwa hivyo mwandishi yeyote wa kazi ya fasihi huandika yale yaliyoujaza moyo wake. Biblia ni kitabu wanachokitumia Wakristo kukuza imani

yao. Kitabu hiki ni muhimu kwani kinahubiri amani, upendo, umoja, mshikamano, heshima, utu wema na fadhili. Sifa hizi ndizo zinazojitokeza pia katika tamthiliya za Emmanuel Mbogo. Wahusika wakuu wamechorwa kwa taswira chanya, kiasi cha kumvutia kila msomaji atamani kuwa kama wao. Mhusika Nyerere ananasibishwa na Nabii Musa katika Biblia (*Nyerere na Safari ya Kanaani*). Kimsingi, watafiti wataelewa sababu za utokezaji wa mwingilianomatini katika utanzu huu wa kidrama. Watabaini kuwa kazi ya fasihi huwa haitoki katika ombwe tupu. Watahitimisha nadharia kuwa, kazi yoyote ya fasihi ni zao la kazi nyingine ya fasihi iliyotangulia. Hili limethibitika kupitia kazi za Emmanuel Mbogo. Kwamba Biblia ndiyo imekuwa chipukizi la kazi zake hizo alizozitunga katika fasihi ya Kiswahili.

### 1.6 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu unakusudia kutazama mwingilianomatini wa Biblia na fasihi katika kazi teule za Emmanuel Mbogo. Sababu kuu iliyotugusa tutazame mada hii ni kwamba watafiti wengi wamechunguza na kuhakiki kazi za Emmanuel Mbogo lakini walikuwa bado kutafiti dhana hii ya mwingilianomatini wa Biblia katika kazi za mtunzi huyu.

Profesa Emmanuel Mbogo ameandika kazi nyingi za fasihi, mathalani tamthiliya, riwaya na hadithi fupi. Miongoni mwa tamthiliya alizoziandika ni *Giza Limeingia*, *Tone la Mwisho*, *Ngoma ya Ng'wanamalundi*, *Sundiata*, *Watoto wa Mama Ntilie*, *Ndoto za Josefu*, *Fumo Liyongo*, tukitaja chache. Kazi zilizozotumika katika utafiti huu ni tamthiliya ya mbili tu; *Nyerere na Safari ya Kanaani* pamoja na *Sadaka ya John Okello* zilizoandikwa na Emmanuel Mbogo (2015). Tuliteua na kuchagua tamthiliya hizi mbili kati ya nyingi alizoandika mwandishi huyu kwani kwa pamoja

zingeweza kutupatia data tulizokuwa tukitafuta kutokana na utafiti wetu na sababu ya pili ilikuwa kwamba, mwingilianomatini wa Biblia katika kazi hizi umejichomoza kwa kiasi kikubwa ukilinganisha na kazi nyingine za mtunzi Emmanuel Mbogo.

## 1.7 Mpangilio wa Tasnifu

Katika tasnifu hii sura ya kwanza imeundwa na vipengele vya kiutangulizi vya utafiti. Vipengele hivyo ni; utangulizi, usuli wa tatizo la utafiti, mihtasari ya kazi teule, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na mpangilio wa tasnifu. Sura ya pili imeundwa kwa vipengele hivi; mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Sura ya tatu imeundwa na mbinu za utafiti. Sura ya nne imeundwa na vipengele vya uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti kisha sura ya tano imeundwa na hitimisho, muhtasari na mapendekezo kuhusu matokeo ya utafiti uliofanyika.

# SURA YA PILI

# 2.0 UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

## 2.1 Utangulizi kwa Jumla

Sura hii inajadili juu ya mapitio ya maandiko yanayohusiana na mada inayofanyiwa utafiti. Tamthiliya ni dhana pana. Katika sura hii tamthiliya ya Kiswahili imejadiliwa kwa mapana na kuona kile kilichosemwa na watafiti waliotangulia. Lengo la sura hii ni kuibua na kujadili usuli wa kinadharia wa masuala ya kinadharia juu ya tamthiliya. Hivyo basi, sura hii inajadili kuhusu dhana ya tamthiliya, mwingilianomatini katika tamthiliya, kazi tangulizi juu ya tamthiliya za Emmanuel Mbogo, pengo la maarifa, kiunzi cha nadharia na hatimaye hitimisho.

## 2.2 Maana ya Tamthiliya na Sifa zake

Mazrui na Syambo (1992) wanaieleza tamthiliya kuwa ni utungo wa fasihi ambao umebuniwa, kwa kiasi kikubwa, kwa lugha ya mazungumzo yenye kuzua na kuendeleza matukio ya hadithi ya utungo huo. Wanaendelea kusema kwamba lugha ya mazungumzo baina ya wahusika ni alama kubwa ya tamthiliya. Dai la wanazuoni hawa kuhusu dhana ya tamthiliya ni kweli. Kwani mazungumzo baina ya wahusika katika tamthiliya hupangwa katika darajia maalum, ambayo imetumika kuutambulisha utanzu huu tofauti na tanzu nyingine. Sambamba na hayo wanasisitiza kuwa chanzo cha matukio ya hadithi ya tamthiliya fulani mara nyingi hupatikana mumo humo katika mazungumzo ya wahusika wake. Hili linalosemwa na wanazuoni hawa ni sahihi. Msomaji wa kazi ya tamthiliya hubaini chanzo cha tukio au kisa fulani kupitia majibizano baina ya mhusika A na mhusika B. Ufafanuzi huu

unaotolewa na wanazuoni, Mazrui na Syambo (1992) kuhusu dhana ya tamthiliya umetufaa sana katika kusogeza mbele utafiti wetu. Kwanza tumebaini kwamba tamthiliya ni tokeo la ubunifu wa msanii. Pili tukio fulani lililotokea katika jamii ndilo huwa kichocheo cha kuibuka kwa kazi hiyo. Kwa mfano mtunzi Emmanuel Mbogo anakiri bayana kuwa kichocheo cha yeye kutunga tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani* ni tukio lililotokea miaka ya 1966. Mgogoro uliotokea baina ya Serikali ya Tanzania chini ya Mhe Julius Kambarage Nyerere na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuhusu sera ya kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa. Wanafunzi wakaipinga sera hiyo na ndipo tafrani ikaanza.

Naye Mulokozi (1999) anafafanua dhana ya tamthiliya kwamba ni kazi iliyokusudiwa kutendwa jukwaani kwa ajili ya hadhira fulani. Anaendelea kusema kwamba, wakati mwingine tamthiliya huitwa mchezo wa kuigiza. Istilahi hii ya tamthiliya imetokana na neno 'mithili' lenye maana ya mfano au ishara ya kitu. Maelezo anayotoa mwanazuoni huyu katika fasihi ya Kiswahili yamebeba mambo makuu ya msingi kuuhusu utanzu wa tamthiliya. Lengo kuu la uandishi wa tamthiliya huwa ni kuchezwa jukwaani ili hadhira fulani iweze kutazama. Wahusika wanaobuniwa katika tamthiliya hizo huwekwa kama kiwakilishi cha wahusika halisi katika jamii. Hivyo watazamaji wakimakinikia tamthiliya huweza kung'amua muhusika anayezungumzwa katika jamii yao.

Vilevile mwanazuoni kutoka nchini Kenya, Wamitila (2003) anasema tamthiliya ni kazi ya kidrama na ya kimaongezi ambayo huigizwa mbele ya hadhira, ni kazi iliyoandikwa ili kusomwa. Nguli huyu anaeleza kuwa, kifani tamthiliya inadhihirika zaidi katika matendo na maonyesho. Mazungumzo baina ya wahusika huchukua

sehemu kubwa katika uwasilishwaji wa maudhui na muundo wake huwa katika dayolojia. Tamthiliya nyingi za Kiswahili zinaakisi fasili hii anayoitoa Wamitila kuuhusu utanzu wa tamthiliya. Tamthiliya zetu teule; *Nyerere na Safari ya Kanaani* na *Sadaka ya John Okello* zinaakisi sifa hizi za kifani.

Kimsingi fasili zilizotolewa na wanazuoni katika aya zilizotangulia hapo juu kuhusu dhana ya tamthiliya zimetusaidia kusonga mbele katika utafiti wetu. Neno tamthiliya usuli wake unaanzia kwenye 'mithili ya' au 'mfano wa'. Tamthiliya hutungwa na kuchezwa jukwaani ili kuwakilisha kitu fulani. Ujenzi wa visa, wahusika na matukio katika kazi hizi za Emmanuel Mbogo uko mithili ya ule wa kwenye Biblia. Ndiyo maana mtu aliyewahi kukutana na Biblia awali akutanapo na kazi hizi kwa mara ya kwanza mwangwi fulani wa Biblia husikika ubongoni mwake paah! Hutaka kujua kama kisa kilichomo humo kinafanana na kile kilichomo kwenye Biblia. Ndiyo maana tukapata swali, Ubiblia unajitokezaje katika kazi za Emmanuel Mbogo?

Mlama (2003) anasema neno "tamthiliya" linatumika kwa maana ya kile ambacho wengine hukiita '*mchezo wa kuigiza'*. Ama kwa hakika tunaona kwamba tamthiliya ni utungo wa kidrama ambao ni aina mojawapo ya sanaa za maonyesho. Tunapomsoma mwanazuoni huyu anagusia dhana ya 'drama' katika fasili aliyotoa. Drama ni kipengele mojawapo katika sanaa za maonyesho, huko magharibi kipera hiki ni maarufu sana. Sifa zake kwa sehemu kubwa zinaingiliana na tamthiliya, ndiyo maana pahala pengine tamthiliya inatambulika kama drama. Kwa hivyo ni kweli kuwa dhana ya drama na tamthiliya zinahusianishwa. Vilevile Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI-2004) wanafasili tamthiliya kuwa ni utungo wa kisanaa ambao

huweka wazo fulani katika matendo na mazungumzo. Kutokana na maelezo haya, tunabaini kwamba tamthiliya ni aina mojawapo ya sanaa za maonyesho ambayo usanii wa utendaji wake hutegemea zaidi vitendo na uongeji, tofauti na aina nyingine kama vile ngoma ambazo hutegemea zaidi uchezaji ngoma na upigaji mziki. Kimsingi tamthiliya ni ule utungo ambao unaweza kuwa umeandikwa au haukuandikwa unaoliweka wazo linalowasilishwa katika umbo la tukio la kuliwezesha kutendeka mbele ya hadhira.

Kwa jumla, fafanuzi zilizotolewa kuhusu dhana ya tamthiliya hapo juu zinaeleza mambo msingi katika kufikia malengo ya utafiti wetu. Zinazungumza kuwa tamthiliya ni utungo wa kisanaa unaotegemea zaidi mazungumzo na matendo ya wahusika. Ndiyo kusema lugha wanayotumia wahusika na yale wanayoyatenda wahusika hao katika kazi husika hubeba dhamira za msingi za kazi husika. Lugha wanayoitumia wahusika huwatambulisha kuwa wao ni watu wa namna gani. Tusomapo kazi za msanii Emmanuel Mbogo tunaona nukuu nyingi za kibiblia zikitumika kupitia vinywa vya wahusika wake. Hili lilitusaidia kubainisha ubiblia unavyojitokeza kupitia kwenye kazi za msanii Mbogo kwa kurejea mazungumzo na matendo baina ya wahusika katika kazi hizo teule; *Sadaka ya John Okello* na *Nyerere na Safari ya Kanaani*.

Tukiendelea kutalii tafiti mbalimbali za wataalam katika uga wa fasihi tunakutana na Aginiwe (2012) anayesema kwamba, tamthiliya ni sanaa ambayo huwasilisha mchezo wa kuigiza katika maandishi au kwa njia ya maandishi. Majina ya wahusika huandikwa katika upande wa kushoto, kisha koloni, kisha maneno ya mhusika. Maelezo ya mwanazuoni huyu yamejikita zaidi kifani yaani umbo la nje la utanzu

huu. Ameeleza umbo la nje la tamthiliya. Fafanuzi hii imetusaidia kung'amua sifa za kifani kuuhusu utanzu wa tamthiliya. Sifa alizozibainisha mtafiti tajwa kuuhusu utanzu wa tamthiliya ni kweli. Tamthiliya za Kiswahili zimeundwa katika fani hiyo. Mbogo (2016) anasema neno 'tamthiliya' linatokana kitenzi 'mithilisha' kwa maana ya kufananisha au kulinganisha. Katika Kiswahili, tamthiliya linatumika kwa maana ya 'michezo ya kuigiza'. Katika tamthiliya huwa kuna ufananishaji ambapo mwigizaji hujifananisha na mhusika wa mchezo wakati wa kuigiza. Tamthiliya huwasilisha mambo kimaigizo kwa kutoa picha ya mambo ambayo yametokea hivyo au yanaaminika yangeweza kutokea hivyo. Tusomapo mawazo ya mwanazuoni huyu tunang'amua kwamba tamthiliya husawiri hali mbalimbali katika maisha ya jamii na ndipo sasa ikaitwa tamthiliya kwa kule kujaribu kufananisha mazungumzo na maigizo hayo. Ni kweli kwamba fasihi husawiri hali halisi katika jamii husika.

Kimsingi fafanuzi zilizotolewa na wanazuoni Aginiwe (2012) na Mbogo (2016) zinaendelea kutueleza kuhusu fani ya tamthiliya ilivyo na jinsi utanzu huo unavyotumika kumithilisha hali mbalimbali za maisha ya jamii. Katika kusogeza mbele utafiti wetu zinatufungulia milango kuielewa vema fani ya tamthiliya na vipengele vilivyomo ndani yake. Katika utafiti tulioufanya tumetumia zaidi vipengele vya kifani ili kubaini ubiblia unavyojitokeza katika kazi za Emmanuel Mbogo sambamba na kueleza sababu za utokezaji wa sifa hiyo kazi kazi teule za mtunzi huyu wa tamthiliya na filamu hapa nchini Tanzania. Kwa jumla, tunaona kwamba tamthiliya ina sifa za kipekee kulingana na maudhui yake na jinsi maudhui hayo yalivyowasilishwa (fani). Hata hivyo, tamthiliya nyingi zina sifa hizi; Utoshelevu kimuundo, tamthiliya nzuri huwa na sehemu tatu muhimu: Mwanzo,

Katikati na Mwisho. Sehemu zake zinatazamiwa kuingiliana, kujengana na kukamilishana. Pili, tamthiliya huwa na lengo. Katika zama za Aristotle, kwa mfano, tanzia ziliwajibika kuzindua hofu na huruma. Tatu, vitendo vyote vinavyofanyika katika tamthiliya vinapaswa kuchangia katika ufanisi wa dhamira za mtunzi. Nne, kifani watunzi wa tamthiliya wanawajibika kutumia mbinu za kisanii zinazowashajiisha wasomaji au watazamaji kuendelea kusoma au kutazamia maatokeo ya matendo yanayoigwa. Mbinu hizo ni pamoja na jazanda, kejeli, ritifaa, tashbihi, tashihisi na uzungumzi nafsia. Wasanii bora ni wale wanaotunga tamthiliya zinazozungumzia kadhia zinazoweza kutimia katika maisha ya binadamu (Mbogo 2016).

Katika utafiti huu imebainika kwamba kigezo kikuu cha kuibanisha tamthiliya ni kuweza kuwasilishwa jukwaani na kutazamwa na hadhira. Tamthiliya huwa na sifa za kawaida za maonyesho ndivyo wanavyosema wanazuoni magwiji katika uga huu wa fasihi; Mhando na Balisidya (1976), Muhando (1983) na Mulokozi (1996). Sifa kuntu zote kuhusu tamthiliya zinajitokeza katika kazi za Emmanuel Mbogo tulizozitalii katika utafiti huu. Tuliegema zaidi kutumia vipengele vya kifani ili kufikia malengo ya utafiti wetu.

## 2.3 Mwingilianomatini katika Tamthiliya za Kiswahili

Katika tamthiliya ya Kiswahili, mwingilianomatini umetafitiwa na wanazuoni mbalimbali. Katika sehemu hii tumetalii na kurejea baadhi ya tafiti zilizokwisha kufanywa katika utanzu huu wa fasihi zikihusisha dhana ya mwingilianomatini. Tumetazama namna watafiti walivyobainisha namna mwingilianomatini ulivyojitokeza katika tamthiliya hizo walizotafiti. Ambrose na wenzake (2015)

walitafiti na kutazama mwingilianomatini katika tamthiliya za Kiswahili. Makala yao ilikuwa na anuani hii ‘Mwingilianomatini katika Tamthiliya za Kiswahili: Mashetani na Kijiba cha Moyo’ katika jarida la *Swahili Forum*. Makala haya yalichunguza viwango na aina za mwingilianomatini baina ya tamthiliya mbili za Kiswahili. Tamthiliya hizo zilikuwa *Mashetani* (Ebrahim Hussein 1971) na *Kijiba cha Moyo* (Arege Timothy 2009). Katika makala haya waandishi wametazama namna tamthiliya hizi mbili zinavyofanana kwa kutumia vipengele vya motifu, maudhui, matumizi ya lugha na wahusika. Wametazama kwa kiasi gani utunzi wa *Kijiba cha Moyo* umeathiriwa na mtunzi wa *Mashetani*. Tamthiliya ya *Mashetani* iliyotunwa mwaka (1971) ndiyo iliyotangulia kuzaliwa na kutungwa.

Kwa hivyo waligundua kuwa Timothy Arege kabla ya kuitunga kazi yake hiyo ya *Kijiba cha Moyo* (2009) alishakutana na kazi ya *Mashetani* na kwa hivyo ikamuathiri katika utunzi wake. Matokeo yaliyopatikana katika utafiti huu ni kweli kwa mujibu wa nadharia ya mwingilianomatini. Kwa mujibu wa nadharia ya mwingilianomatini kazi za fasihi zinaingiliana na kuathiriana kwa namna mbalimbali. Nadharia hii ilitufaa katika utafiti huu hakika. Tuliuendea utafiti wetu kwa ujasiri na moyo mkuu tukijua kwamba athari ya kazi tangulizi ni nadra kukosekana kwenye kazi zinazofuata, hasa zile alizokutana nazo mtunzi au mwandishi wa kazi husika tunazotafiti. Mningo (2015) katika tasnifu yake ya uzamili, *“Tathimini ya Mwingilianomatini katika Utunzi wa Emmanuel Mbogo: Utafiti Linganishi wa Tamthiliya ya Ngoma ya Ng’wanamalundi na Fumo Liyongo.”* Lengo kuu la utafiti huo lilikuwa ni kufanya tathmini ya mwingilianomatini katika utunzi wa Emmanuel Mbogo, kwa kulinganisha tamthiliya ya *Ngoma ya Ng’wanamalundi* (1988) na *Fumo*

*Liongo* (2009). Tuliposoma utafiti huu tulibaini jinsi mtunzi huyo, Emmanuel Mbogo anavyofumbata mbinu ya mwingilianomatini katika kazi zake za fasihi, na namna mbinu hiyo inavyotumika kuibua dhamira za tamthiliya hizo. Kupitia utafiti huu wa Mningo tunaona kwamba Emmanuel Mbogo ameathiriwa mno na mbinu ya mwingilianomatini. Anaitumia zaidi mbinu hii katika utunzi wa kazi zake mbalimbali za fasihi mathalani tamthiliya, riwaya na filamu.

Bosibori (2016), katika tasnifu yake ya shahada ya uzamili yenye jina, "*Mwingilianomatini kati ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mstahiki Meya"* ametafiti na kuonyesha namna mwingilianomatini unavyojitokeza katika tamthiliya hizo mbili, *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* (Gogol, 1979) na *Mstahiki Meya* (Arege, 2009). Katika tasnifu yake hii mtafiti huyu ameonyesha namna tamthiliya hizi mbili zinavyoingiliana kifani na kimaudhui. Amebainisha mwingilianomatini unavyojitokeza kwa kutumia vipengele mbalimbali vya kifani na kimaudhui akivitazama kwa mwega wa nadharia ya mwingilianomatini. Bosibori amehitimisha kuwa, kazi takribani zote za kifasihi, huingiliana kifani na kimaudhui.

Tunaona kwamba madai haya anayoyatoa Bosibori ni kweli na yanaungwa mkono na wanazuoni wengine katika uga huu wa fasihi, hasa katika dhana ya mwingilianomatini. Kuna dai kwamba kazi za fasihi hukamilishana, hutoshelezana. Hiki anachosema Bosibori katika tasnifu yake hii kinathibitika na kilitusaidia kusonga mbele katika kuuendea utafiti wetu. Kwa jumla, mwimgilianomatini katika tamthiliya ya fasihi umeshaanza kutafitiwa na wanazuoni kutoka pahala pengi ulimwenguni kama tulivyoona kazi hizo tangulizi hapo juu. Mada lengwa inayofanyiwa utafiti humu ndiyo inaleta upya kwamba inazungumzia kitu kipya

ambacho watafiti wengine bado hawajakizungumza katika tafiti zao, mwingilianomatini kati ya Biblia na fasihi. Kimsingi katika tasnifu hii tumebainisha mwingilianomatini wa Biblia ulivyojitokeza katika kazi teule za Emmanuel Mbogo. Sambamba na hilo tumeeleza sababu za kujitokeza kwa mwingilianomatini huo katika kazi hizo; tamthiliya za *Nyerere na Safari ya Kanaani* na *Sadaka ya John Okello*.

## 2.4 Wasifu wa Emmanuel Mbogo

Emmanuel Mbogo ni mtunzi na mwandishi wa tamthiliya, riwaya na hadithi fupi. Yeye ndiye aliyeandika tamthiliya hizi mbili tulizozitumia katika utafiti wetu, *Nyerere na Safari ya Kanaani* na *Sadaka ya John Okello*. Ni msomi na profesa katika uga wa sanaa za maonyesho, filamu na fasihi ya kiswahili. Mningo (2015) katika tasnifu yake ya shahada ya uzamili alipata wasaa wa kufanya usaili na msanii huyu. Kupitia kazi yake tuliweza kupata usuli wa maisha ya mtunzi Emmanuel Mbogo na taarifa zake kuhusu utunzi kwa ujumla.

Mtunzi huyu, Emmanuel Mbogo alizaliwa tarehe 01/03/1947 katika wilaya ya Kongwa, mkoa wa Dodoma. Alisoma katika shule ya msingi Mpwapwa na kuhitimu darasa la nane mwaka 1963. Baadaye alijiunga na masomo ya sekondari katika shule ya sekondari Indian (kwa sasa inajulikana kama Shule ya Sekondari Dodoma) na kuhitimu mwaka 1967. Wakati akisubiri matokeo yake, ya mtihani wa Sekondari alifanya kazi ya ukarani katika Wizara ya Kilimo, mkoani Dodoma. Baada ya kufaulu mwaka 1968, alijiunga na Chuo cha Ualimu Morogoro kwa ajili ya mafunzo ya Ualimu daraja la IIIA na kuhitimu mwaka 1969. Akiwa chuoni hapo, ndipo alipogundua kipaji chake cha uandishi. Hii ni baada ya kuandika hadithi aliyoiita

*James I Die of Love* (1968) katika jarida la chuo lililokuwa linaitwa *Morani*. Hadithi hiyo iliwavutia wasomaji na kusifiwa sana na mwalimu wake wa Fasihi ya Kiingereza na wanachuo wenzake. Emmanuel Mbogo anakiri kuwa hadithi hiyo ndiyo iliyomtanabaisha uwezo wake wa kutunga hadithi na hivyo kupata hamasa na ari ya kuingia katika ulimwengu wa utunzi.

Mwaka 1970 alipangiwa kufundisha katika shule ya msingi Mwitikila iliyopo mkoani Dodoma. Alipokuwa akiendelea kufanya kazi alipata fursa ya kujiunga na chuo kimoja huko Uingereza kilichofahamika kama Rapid Result College. Alikuwa akisoma kwa mfumo wa elimu ya masafa. Alisoma masomo ya Jiografia na Kiswahili na lengo lake likiwa kuongeza alama stahiki kwa ajili ya kujiunga na masomo ya stashahada. Wakati huo akiwa katika shule hiyo, alitunga tamthiliya yake ya kwanza iliyoitwa *'Mama Tamasha'* (1970). Mnamo mwaka 1971 alihamia shule ya msingi Nara. Akiwa shule hiyo aliufanyia mazoezi mchezo huo na wanafunzi wake darasani, lengo likiwa kusikiliza namna unavyosikika katika mazungumzo na vitendo. Mchezo huo uliigizwa jukwaani mwaka 1972 alipokuwa akifundisha shule ya msingi Bwigiri. Wakati huo akiwa na kundi lake la waigizaji (wanafunzi wake) walitembea na kuuigiza mchezo huo katika vijiji mbalimbali vya ujamaa vilivyokuwepo wakati huo. Mwaka huohuo wa 1972, mtunzi huyu aliubadili jina mchezo huo na kuuita '*Watoto Wetu*.'

Mnamo mwaka 1973 Emmanuel Mbogo alijiunga na masomo ya stashahada ya ualimu na sanaa za maonyesho katika chuo cha ualimu Chang'ombe, kilichopo jijini Dar es Salaam na kuhitimu mwaka 1974. Baada ya kuhitimu mafunzo ya ualimu ngazi ya stashahada alipangwa kufundisha katika Chuo cha Ualimu Katoke, ambako

alifundisha hadi mwaka 1976 Juni alipojiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kusoma shahada ya kwanza na ya pili katika sanaa za maonyesho (BA in Theartre Arts and MA in Thearter Arts). Emmanuel Mbogo akiwa chuo kikuu cha Dar es Salaam alitunga tamthiliya yake ya pili iliyoitwa *Giza Limeingia* (1980) na kisha akaandika nyingine iliyoitwa *Tone la Mwisho* (1981). Alipokuwa masomoni chuo kikuu cha Dar es Salaam alipata fursa zaidi ya kung'arisha kipaji chake kuhusu sanaa na utunzi. Kwa kudra za Mwenyezi Mungu, msanii huyu akahitimu masomo yake ya shahada ya pili katika Sanaa za Maonyesho mwaka 1981. Mwaka uliofuata wa 1982 alipata fursa ya kwenda kujiendeleza kimasomo huko nchini Ujerumani, Chuo Kikuu cha Humboldt kilichokuwepo Berlin kwa masomo ya shahada ya tatu katika sanaa za maonyesho (PhD in Theatre Arts) na hatimaye kuhitimu mwaka 1984.

Msanii huyu baada ya kuhitimu masomo yake huko nchini Ujerumani, alirudi nchini Tanzania na kupata fursa ya kufanya kazi katika Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) ambayo kwa sasa inatambulika kama Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI). Taasisi hii ipo Chuo Kikuu cha Dar es. Alifundisha hapo toka arejee kutoka Ujerumani mpaka mwaka 1989. Mwaka 1990 alienda nchini Kenya ambako alipata nafasi ya kufundisha Chuo Kikuu cha Moi hadi mwaka 1991. Mwaka 1991 Emmanuel Mbogo alihama kutoka Chuo Kikuu cha Moi na kwenda kufundisha Chuo Kikuu cha Maseno, kilichopo Kisumu nchini Kenya hadi mwaka 2002. Kwa hakika Emmanuel Mbogo ametumika kwa muda mwingi nchini Kenya. Mwaka 2003 alihamia Chuo Kikuu cha Kenyata ambapo alifundisha huko hadi mwaka 2006. Baadaye mwaka 2007, Emmanuel Mbogo alikwenda nchini Rwanda na kufundisha Chuo Kikuu cha Kigali, kwa muda wa mwaka mmoja. Kuanzia mwaka 2008

Emmanuel Mbogo aliporudi nchini Tanzania alijiunga na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, ambapo yupo hadi sasa kama mhadhiri chuoni hapo akifundisha kozi mbalimbali za fasihi, filamu na sanaa za maonyesho. Mtunzi wetu huyu tuliyechagua kutumia kazi zake katika utafiti wetu, Emmanuel Mbogo ameshatunga, kuandika na kuchapisha kazi mbalimbali za Fasihi; riwaya, tamthiliya pamoja na hadithi fupi. Tamthiliya alizokwisha tunga na kuzichapisha ni hizi zifuatazo; *Watoto Wetu* (1972), *Giza Limeingia* (1980), *Tone la Mwisho* (1981), *Morani* (1983), *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1988), *Fumo Liyongo* (2009), *Sundiata* (2011), *Sadaka ya John Okello* (2015), *Nyerere na Safari ya Kanaani* (2015), *Wangari Maathai* (2015), *Nyota ya Tom Mboya* (2016), *Mondlane na Samora* (2016), *Malkia Bibi Titi Mohamed* (2016) pamoja na *Ndoto za Josefu* (2016-Bado haijachapishwa).

Katika utanzu wa riwaya mwandishi huyu ameandika na kuchapisha kazi mbalimbali. Riwaya ambazo ameandika mtunzi huyu na kuzichapisha ni hizi zifuatazo; *Watoto wa Mama Ntilie* (2002), *Vipuli vya Figo* (2008) na *Siri za Maisha* (2010). Ndani ya riwaya hizi mfasihi huyu amezungumza mambo mengi yanayoihusu hasa jamii ya kitanzania katika nyuga mbalimbali za kimaisha mfano; uchumi, siasa na kiutamaduni. Katika utafiti wetu tulichagua kutumia tamthiliya mbili tu za mtunzi huyu Emmanuel Mbogo, *Sadaka ya John Okello* (2015) na *Nyerere na Safari ya Kanaani* (2015) kama ilivyojadiliwa katika sura zilizotangulia. Kwa hivyo mjadala wetu utajikita tu katika tamthiliya hizi teule mbili tu. Tulichagua tamthiliya hizi mbili kwa maksudi kabisa kwa sababu ndizo zingeweza kutupatia data za utafiti wetu kwa kiwango kikubwa zikilinganishwa na kazi nyingine zilizoandikwa na mtunzi huyu.

## 2.5 Muhtasari wa Tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani*

*Nyerere na Safari ya Kanaani*, ni tamthiliya iliyotungwa na Profesa Emmanuel Mbogo, mwaka 2015. Tamthiliya hii ina sura ya kihistoria. Mtunzi katika sehemu ya utangulizi kuhusu tamthiliya hii anatujuza kuwa asili ya tamthiliya hii ni mgogoro mkubwa wa kihistoria uliozuka kati ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Muhimbili. Mgogoro huu ulizuka mnamo mwezi Oktoba, mwaka 1966. Wanafunzi hawa walifanya maandamano makubwa hadi Ikulu wakipinga vikali sera ya kuwataka kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT). Mgogoro huo ulipelekea msuguano mkubwa uliopelekea wanafunzi hao walioandamana kufukuzwa chuo, warudi kwao wakalime.

Tamthiliya hii inadokeza kwa sehemu kuhusu mgogoro huo na mwandishi anafikiri kuwa kwa sehemu kubwa mgogoro huo ulichangia katika kukuza mimba ya safari ya Kanaani, nchi ya maziwa na asali hapa Tanzania na kiongozi ama dereva wa safari hiyo akiwa Mwalimu Nyerere. Ni tamthiliya nzuri hakika. Inawafaa wengi, wanahistoria, wanafasihi, watawala n.k. Kwa kutumia mkabala wa usomaji makini tuling’amua kuwa tamthiliya hii imejengwa kutoka pande mbili zinazokinzana. Pande hizo ni serikali ya Tanzania chini ya Rais Julius Kambarage Nyerere na upande wa pili ni serikali ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Muhimbili chini ya rais wao Martin. Kiini cha mgogoro huo katika tamthiliya hii ni sera ya serikali ya Tanzania inayowataka vijana wote watakaomaliza elimu yao ya chuo kikuu kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwa muda wa miezi sita kabla ya kuajiriwa. Martin, Saigoda na Farida ndiyo wanaosimama kidete mstari wa mbele kuwaongoza wenzao kupingana na sera hii dhalimu kwa mtazamo wao.

Ndani ya tamthiliya hii mtunzi amebainisha tofauti zinazoweza kujitokeza katika jamii baina ya watawala na watawaliwa. Rais wa Tanzania, Mwalimu J.K Nyerere anawakilisha tabaka la watawala ambao huwa na maono fulani mazuri kwa fikra zao kuhusu jamii wanazoziongoza ili kuziendeleza lakini huishia kupata mapingamizi kutoka kwa wanajamii wasioelewa ama wasiotaka kuambatana na maono na maamuzi hayo ya watawala wao. Martin, Saigoda na Farida wanawakilisha tabaka tawaliwa ambao hawako tayari kushikamana na maono hayo mageni yanayoletwa na watawala wao.

Mtunzi amemchora mhusika, Mwalimu Nyerere kama kiongozi ambaye anataka kuipeleka nchi yake katika maendeleo ya kiwango cha juu. Mhusika huyu amefananishwa na Nabii Musa kutoka huko Israel anayesemekana kuwaongoza watu wa taifa lake kutoka utumwani Misri na kurejea nchini mwao Kanaani, nchi Mungu aliyowaahidia kwamba atawapa kuwa urithi wao. Pamoja na uongozi wa nabii huyo kuwa mwema lakini hakubahatika kuingia Kanaani kutokana na kukiuka baadhi ya makatazo ya Mwenyezi Mungu. Tukimnukuu mhusika mmoja wapo anasema,

**KAMBONA**: Ndiyo maana watu mitaani wanakuita Nabii Musa. Unataka kutupeleka Kanaani kunako nchi ya asali na maziwa.

Chanzo: Data za Utafiti katika *Nyerere na Safari ya Kanaani* (uk 14)

Kwa jumla tamthiliya hii imeeleza kuhusu nchi ya Tanzania na changamoto mbalimbali ilizopitia toka kupata huru kuyaendea maendeleo chini ya kiongozi wake wa awamu ya kwanza Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Sera mpya mbalimbali hazikupokelewa vema pengine kutokana na wananchi kutokujuzwa vema kuhusu

sera hizo. Kwa mfano sera ya JKT, sera ya ujamaa na kujitegemea na nyinginezo nyingi.

## 2.6 Muhtasari wa Tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello*

*Sadaka ya John Okello* ni tamthiliya ya kihistoria. Mtunzi wa tathiliya hii ni mwandishi nguli katika sanaa za maonyesho na filamu hapa nchini Tanzania, Emmanuel Mbogo. Ilitungwa na kuchapishwa kwa mara ya kwanza mwaka 2015, Dar es Salaam. Tamthiliya hii inaeleza kuhusu mapinduzi yaliyofanyika Visiwani Zanzibar mnamo mwaka 1964 Januari 12. Historia inasema, kabla ya mkoloni Muingereza kuondoka visiwa vya Zanzibar, alikabidhi mamlaka ya kuitawala Zanzibar kwa Waarabu, chini ya Sultan Jamshid.

Tendo hili lilifanyika mnamo mwaka 1963 Januari 12. Wazawa wengi visiwani humo, waafrika kwa pamoja, waliona kuwa uhuru huo ulikuwa wa bandia. Mtunzi anaonyesha namna mapinduzi yalivyofanyika na watu mbalimbali waliohusika kufanikisha mapinduzi hayo. Ni tamthiliya nzuri ya kihistoria kwa kweli. Wahusika katika tamthiliya hii wamepewa majina ya watu halisi waliokuwepo wakati huo mapinduzi yakifanyika. Kwa hivyo, mtu atakapo kujua ama kufahamu kwa kina kuhusu historia ya mapinduzi visiwani Zanzibar asomapo tamthiliya hii atafaidika zaidi na atang’amua mengi. Kiongozi mkuu aliyesimamia mapinduzi hayo ni Field Marshall John Okello, kijana kutoka Uganda. Mtunzi wa tamthiliya hii ameijenga kazi hii yake hii kwa kuegema zaidi kwenye tukio la mapinduzi lililofanyika visiwani Zanzibar mwaka 1964. Wahusika wake wamechorwa na kuvikwa sura mbalimbali walizozionyesha Waafrika baada ya mkoloni Mwingereza kukabidhi uhuru kwa wageni, waarabu chini ya Sultan Jamshid na kuwasahau wazawa. Tukio

hili lilipingwa na wazawa wengi. Hata hivyo tunapoisoma tamthiliya hii kwa mkabala wa usomaji makini tunaona kuwa pamoja na waafrika wengi kutoridhika na uhuru huu bandia ambao waliachiwa na mwingireza yaliibuka mawazo tofauti tofauti namna ya kupambana na uonevu huu. Mhe. Karume kama tunavyomuona kwenye tamthiliya hii chini ya chama cha siasa cha Afro Shiraz Party (ASP) aliamini kuwa njia pekee ya kupambana na ujangili huo ilikuwa sanduku la kura. Abdulrahman Babu-Umma Party naye alikuwa na falsafa zake za kikomunisti sambamba na mwenzao Shamte.

Kundi lililofanya mapinduzi ni kundi lililoongozwa na kijana kutoka Uganda, Field Marshal John Okello. Haya ndiyo tuliyoyaibua katika tamthiliya hii tulipokuwa tukifanya utafiti. Hata hivyo mtunzi kidhamira anaelekea kutujuza kwamba, umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Anaifundisha jamii umuhimu wa kuungana na kuwa wamoja wanapopambana na adui wa namna yoyote ile. Jamii ikishikamana na kuwa moja yaweza kufaulu katika mapambano yote inayoyafanya. Dhamira nyingine inayoibuliwa katika tamthiliya hii ni umuhimu wa kujitoa muhanga, kufa au kupona tunapotaka kuleta mabadiliko ya kweli na yenye tija kwa jamii zetu. Hili linatakiwa haswa kwa viongozi wetu wanaosimama mbele za wananchi katika nyadhifa mbalimbali.

Wanatakiwa kuwa na moyo huo wa ushujaa na kukubali kujitolea kwa namna yoyote popote inapobidi ili kuleta maendeleo ya kweli. John Okello, muhusika mkuu katika tamthiliya hii amechorwa kuonyesha taswira hiyo. Amefanya kwa nafasi yake. Ameongoza jeshi la vijana wenzake na hatimaye amefanikiwa kupata uhuru wa kweli, japo baadaye anasalitiwa na kufukuzwa kutoka ardhi ya Zanzibar kwa kigezo

kuwa si mzawa. Ni tamthiliya nzuri sana ya kihistoria. Jamii inaweza kung'amua mengi yanayohusu mapinduzi yaliyotukia mwaka wa 1964. Tumechagua tamthiliya hii kwa lengo mahsusi kabisa kuwa itaendana na utafiti wetu tunaoufanya. Utafiti wetu unatumia nadharia ya mwingilianomatini, kwa hivyo hata hoja zitakazoibuliwa kutoka katika tamthiliya hii kwa mkabala wa mwingilianomatini.

## 2.7 Kazi Tangulizi Kuhusu Tamthiliya za Emmanuel Mbogo

Kazi za Emmanuel Mbogo zimetafitiwa na wanazuoni mbalimbali katika uga wa fasihi hapa nchini Tanzania na barani Afrika kwa jumla. Watafiti hao wametazama mada mbalimbali katika kazi za mwandishi huyu. Katika sehemu hii tumetazama kazi zilizofanywa na watafiti katika kazi za Emmanuel Mbogo. Tulirejea katika tafiti hizo ili kuweza kubaini pengo la maarifa ili tuuendee utafiti wetu kwa weledi. Katika sehemu inayofuata hapa chini tumetazama tafiti mbalimbali zilizofanywa kuhusu kazi za Emmanuel Mbogo.

Kwa kuanza tumtazame Mosoti (1993). Huyu amehakiki maudhui katika tamthiliya nne za Emmanuel Mbogo; *Giza Limeingia* (1980), *Tone la Mwisho* (1981), *Watoto Wetu* (1981) na *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1988). Amehakiki tamthiliya hizi katika misingi ya nadharia ya uyakinifu wa kijamaa. Miongoni mwa maudhui aliyoyahakiki ni pamoja na dhamira za ukombozi, dhuluma, usaliti, ubinafsi na nafasi ya mwanamke katika jamii. Dhamira hizi alizoziibua mtafiti huyu katika utafiti wake alioufanya zinadhihirika hakika katika kazi hizo. Yale yaliyozungumzwa na mtunzi wa kazi alizozitafiti Mosoti (1993) yalionekana yakini. Hata hivyo katika utafiti huu alioufanya Mosoti tunaona kwamba amejikita zaidi upande wa maudhui, sehemu ya fani haikuguswa. Kwa hivyo, tulibaini pengo hapa katika sehemu ya fani.

Tasnifu hiyo ilitusaidia kusogeza mbele utafiti wetu hasa kwa kutaka kushughulika na sehemu ya fani ambayo haikuguswa bado katika kazi za Emmanuel Mbogo.

Mtafiti mwingine aliyezamia kazi za Emmanuel Mbogo ni Shemweta (2015), katika tasnifu yake ya shahada ya uzamili katika fasihi ya kiswahili yenye jina, *"Itikadi katika Tamthiliya za Emmanuel Mbogo: Utafiti Linganishi wa Ngoma ya Ng'wanamalundi na Fumo Liyongo."* Shemweta anaeleza kwamba katika tamthiliya za *Ngoma ya Ng'anamalundi* na *Fumo Liyongo* kuna itikadi mbalimbali zinazohusiana na maisha ya kila siku ya jamii ya Kitanzania. Itikadi hizo ndizo zinazoongoza maisha ya kila siku ya jamii hizo. Itikadi mojawapo iliyojitokeza zaidi katika kazi hizi ni itikadi ya ushirikina. Hali hii inaonyesha kuwa katika jamii alizoziandikia mwandishi itikadi ya ushirikina ilikuwa imeota mizizi kwa kiasi kikubwa. Tulipoisoma kazi hii ya mtafiti huyu dhana ya mwingilianomatini wa Biblia na fasihi haijaguswa, kwa hivyo ikatupa dira ya kufanya uchaguzi sahihi wa mada mpya utafiti katika kazi za Emmanuel Mbogo.

Clemence (2015), alitazama mbinu za kitanzia za Kiaristotle katika tamthiliya za *Fumo Liyongo* na *Sundiata*. Katika tasnifu yake ya uzamili yenye anuani, "Kuchunguza Mbinu za Kitanzia za Kiaristotle katika Tamthiliya za Fumo Liyongo na Sundiata" anabainisha kwamba, mtunzi Emmanuel Mbogo ametumia kwa kiasi kikubwa mbinu za kitanzia za Kiaristotle katika kazi zake hizo. Tunaposoma utafiti huu tunabaini kwamba mtunzi Emmanuel Mbogo anajipambanua waziwazi kama mtunzi wa tamthiliya za Kiswahili kwa mtindo wa Kiaristotle. Clemence ameonesha namna mtindo wa Kiaristotle ulivyotumika sambamba na mbinu za kijadi na bado tamthiliya ikatunza taswira yake. Katika utafiti huu mtafiti amebainisha sifa

mbalimbali za kitanzia za kiaristotle zinazojitokeza kwenye kazi za Emmanuel Mbogo; Tamthiliya za *Fumo Liyongo* na *Sundiata*. Ndani ya kazi hii tumepata maarifa kuhusu dhana ya mwingilianomatini inavyoweza kujitokeza katika kazi za fasihi na hivyo tukashajiisha utafiti wetu. Mtafiti Clemence (ameshatajwa) ameonyesha namna mwingilianomatini ulivyojitokeza katika kazi hizo alizotafiti.

Bwelele (2016) alitafiti vipengele mbalimbali vya kimtindo katika kazi za Emmanuel Mbogo. Katika utafiti wake alitumia tamthiliya za *Nyerere na Safari ya Kanaani* na *Sadaka ya John Okello*. Tulipokuwa tukisoma utafiti wa mwanazuoni huyu tulibaini kwamba, kuna mfanano mkubwa wa vipengele vya kimuundo kati ya tamthiliya hizo mbili alizozitafiti. Tunasoma kuwa mfanano huo unathibitika kupitia vipengele vya wahusika, taswira, matumizi ya ucheshi na kuchanganya tanzu. Andiko lake lina anuani hii, *"Kuchunguza Mtindo katika Tamthiliya za Sadaka ya John Okello na Nyerere na Safari ya Kanaani."*

Mtafiti huyu ametafiti tamthiliya teule katika utafiti; *Nyerere na Safari ya Kanaani* na *Sadaka ya John Okello* lakini dhana ya mwingilianomatini haikuguswa. Kazi ilitufaa sana katika kusogeza mbele utafiti wetu kwa namna nyingi. Kwanza kwa kutupa maelezo ya msingi kuhusu tamthiliya mbili tulizokuwa tukizitafiti ambazo nazo zilishughulikiwa na mtafiti huyu. Pili utafiti ulikuwa rejeo muhimu sana katika kuukamilisha utafiti huu kwa kubaini mtindo wa Kiaristotle uliokuwa umetumika katika kazi hizi za Emmanuel Mbogo. Na mwisho dhana ya ubiblia haikuguswa katika utafiti huu, hivyo tukabaini pengo na kutamani kuliziba kwa kufanya utafiti wa kazi hizi kwa kutumia muktadha wa kimwingilianomatini.

## 2.8 Pengo la Maarifa

Kutokana na maandiko mbalimbali tuliyopitia kutoka vyanzo vya maarifa, hatukuona andiko lililoshughulikia ubiblia katika kazi za Emmanuel Mbogo kwa jumla. Hivyo tumeona ni vema tushughulikie uga huu ili kuweza kuziba pengo la kitaaluma lililoachwa wazi na wanazuoni mbalimbali waliochunguza kazi mbalimbali katika fasihi ya Kiswahili.

## 2.9 Mkabala wa Kinadharia

Uhakiki wowote unapofanyika shurti uongozwe na nadharia fulani mahsusi. Ili kufanya zoezi la uhakiki lifanyike kwa weledi zaidi, pameibuka nadharia mbalimbali zinazotoa mwongozo au misingi ya kufanya uhakiki wa kazi za fasihi. Ndiyo kusema, uhakiki wowote unaofanyika katika zama hizi shurti uongozwe na nadharia au ujiegemeze kwenye mkondo fulani wa mawazo. Katika uga wa fasihi pamekuwepo nadharia nyingi zinazotumiwa na wanazuoni katika uga huu kufanya uhakiki wa kazi za fasihi.

Miongoni mwa nadharia hizo ni hizi zifautazo; nadharia ya ufeministi, nadharia ya uigizaji, nadharia ya umuundo, nadharia ya uhalisia-Nafsi, nadharia ya kimax, nadharia ya udenguzi, nadharia ya mguso, nadharia ya kihemenitiki, nadharia ya umbuji, nadharia ya ubunilizi na nadharia ya mwingilianomatini. Mlaga (2010), anasema, "Nadharia ni maelezo ya jambo ambayo hufungamana na vigezo vilivyowekwa kutokana na majaribio mengi yaliyofanywa katika nadharia hiyo." Mlaga anaendelea kusema kwamba, nadharia yaweza kutokana na mawazo yaliyoundwa kitambo na jopo la wataalam. Fafanuzi ya mwanazuoni huyu inatuelekeza kwenye dhana kuwa maelezo hayo juu ya dhana husika lazima yatokane

na majaribio yaliyofanyika mara nyingi ili kubaini ukweli. Wamitila (2003), anaifafanua dhana ya nadharia kama kauli au kaida za kijumla zinazotegemezwa kwenye kufikiri kwa namna fulani na kwamba, kaida hizo huweza kutumika kueleza jambo fulani. Ufafanuzi wa mwanazuoni huyu nguli katika uga wa fasihi kuhusu dhana ya fasihi unatufundisha kuwa, nadharia ni mawazo ama misingi iliyoegemezwa katika kaida fulani, lakini mawazo haya yanatumika kufanya fafanuzi au kutoa maelezo kuhusu jambo fulani. Kutokana na fafanuzi za wanazuoni hawa, tunapata ukweli kuwa, nadharia ya fasihi ni mwongozo unaomwelekeza ama unaomwongoza msomaji wa kazi ya fasihi katika vipengele vyake vyote. Nadharia hii yaweza kutokana na usomaji wa kazi za fasihi wa mtu binafsi au jopo la wanazuoni. Nadharia ya Fasihi inajidhihirisha zaidi katika uhakiki wa kazi za fasihi.

### 2.9.1 Nadharia ya Mwingilianomatini

Utafiti wetu uliongozwa na nadharia ya Mwingilianomatini. Nadharia ya Mwingiliaomatini iliasisiwa na Mikhail M. Bhakhtin. Mwanazuoni huyu alikuwa mwanaisimu na mhakiki wa kazi za fasihi aliyeishi kati ya 1895 hadi 1975 (Njogu, Chimerah na Wafula 2007). Mwega wa nadharia hii wadai kuwa, ili hadhira ielewe kazi yoyote ya fasihi lazima ihusishe vipengele vingine nje ya muktadha wa usomaji au usimulizi ule. Dhana ya kuingiza vipengele hivyo ndiyo huitwa mwingilianomatini. Nadharia hii pia hujulikana kama nadharia ya usemezano. Bakthin aliamini kwamba kazi ya fasihi ina sauti mbalimbali zinazoingiliana na kupiga mwangwi katika kazi nyingine zilizotangulia, zilizopo na zitakazo kuja baadaye. Mwanazuoni huyu anaamini pia kuwa utanzu wa riwaya katika fasihi una uwezo wa kuingiza vipengele vingine lakini ukabaki na sifa zake kama utanzu.

Kutokana na mawazo haya ya Bakhtin tunajifunza kwamba, utanzu wa fasihi kuwa na vipengele vingine vya fasihi hakuondoi sifa ya utanzu huo. Mwingiliano anaosema mhakiki huyu ni huu, yaani kazi moja ya fasihi kuwa na sifa za tanzu nyingine ndani yake. Dhana ya mwingilianomatini hurejelea pia uhusiano uliopo kati ya matini husika na nyingine ambazo msomaji au mwandishi amekutana nazo. Wanafasihi wanakubaliana kuwa, Matini za fasihi huingiliana na kutegemeana.

Mwingilianomatini ni nadharia ya fasihi. Nadharia hii imepata kuhusishwa na mnadharia wa Kifaransa, Julia Kristeva, ambaye aliizua kutoka kwenye nadharia ya Usemezano ya Mikhail Bakhtin. Dhana hii hutumika kuelezea kuwepo kwa sifa mbalimbali za matini moja au zaidi katika kazi za fasihi. Kama nadharia ya fasihi, mwingilianomatini huchukulia kwamba, kazi ya Fasihi inahusiana na kazi iliyoandikwa kabla kwa namna moja ama nyingine. Charney na Plotell (1978), wanasema kuwa, nadharia ya mwingilianomatini inajikita kwenye msingi kuwa matini ya kisanaa si zao la mwandishi pekee bali ni zao la jinsi matini inavyohusiana na matini nyingine na miundo ya lugha yenyewe. Wanaendelea kusisitiza kwamba, dhana hii husisitiza kwa matini zote za kisanaa zaweza kuchukuliwa kama matini moja kuu ambazo hujibizana, kila moja ikisemezana na nyingine. Wanakubaliana kuwa matini hutegemeana ili kuzalisha maana. Baadhi ya Mihimili Mikuu ya Nadharia ya Mwingilianomatini kwa mujibu wa Julia Kristeva ni hii ifuatayo kama tulivyoibainisha hapa chini.

i. Matini yoyote ile ni mabadiliko ya mpangilio wa matini nyingi tangulizi.
ii. Kazi ya Fasihi huundwa kutokana na mifumo ya kanuni na tamaduni mbalimbali zilizowekwa na kazi tangulizi za Fasihi. Kwamba taswira za

maisha ya kawaida na uhusiano wa kimaana huunganishwa na kubadilishwa.

iii. Matini moja hufafanua usomekaji wa mkusanyiko wa matini zote za kongoo moja, ambapo matini tangulizi hufyonzwa na kujibiwa na matini mpya

iv. Matini za Fasihi huwa zimechota, kunukuu, kugeuza, kuiga kwa namna ya kubeza au kurejelea kwa njia moja ama nyingine matini nyingine.

v. Kila usomaji wa matini huwa ni kijalizo cha matini tangulizi, na hivyo basi huigeuza kuwa kiwango. Kwa jinsi hii kauli inayonukuliwa hubadili na kuelezea upya kauli asilia kwa kuiambatisha na muktadha mwingine wa kiisimu na kijamii.

Kwa jumla, nadharia ya mwingilianomatini, mwasisi wake ni Mikhail Bakhtin, mwanaisimu na mhakiki na mwendelezaji wake ni Julia Kristeva. Bakhtin (1981) alishikilia kwamba kazi ya fasihi huwa na sauti mbalimbali zinazoingiliana na kutoa mwangwi wa kazi nyingine zilizotangulia, zilizopo na zitakazo kuja baadaye. Ndiyo kusema, kazi ya Fasihi ya mwingiliano huwa na uwezo wa kuhusiana, kuingiliana na kurejeleana na kazi nyingine za fasihi kwa njia tofauti. Kauli ya mwangwi katika nadharia hii inatumika kumaanisha kwamba, matini moja ya Fasihi inamrejesha msomaji katika matini nyingine aliyotangulia kuisoma au kusimuliwa pahala na labda kumsaidia kuielewa kwa urahisi zaidi matini anayoisoma sasa. Dhana ya mwingilianomatini katika fasihi ya Kiswahili, imejadiliwa na wataalam mbalimbali. Miongoni mwao ni Wamitila (2002), Wamitila (2008), Senkoro (2011), Herman (2011) na Adam (2014). Wamitila (2008) anaiangalia dhana ya mwingilianomatini

kwamba ni kuhusiana na kutegemeana kwa matini au kazi za Fasihi na matini au kazi za Fasihi zilizotangulia. Uhusiano huo huweza kutazamwa katika vipengele vya fani na maudhui. Profesa wa fasihi ya Kiswahili, Senkoro (2011) anaielezea mbinu ya mwingilianomatini kuwa, ni kule kutumiwa kwa utanzu mmoja wa fasihi katika kutolea au kuwasilishia utanzu mwingine, mfano wimbo ndani ya ngano au hadithi. Anaongezea hoja yake kwa kusema kuwa, pia ni ule uwepo wa sifa mbalimbali za matini moja au zaidi katika kazi fulani ya fasihi, mfano matumizi ya nyimbo, barua, ngoma, masimulizi ya hadithi, misemo na nahau.

Mtaalamu mwingine ni Bakize (2011), ambaye anaielezea mbinu ya mwingilianomatini kama mtindo wa kuchanganya vipengele mbalimbali vya kisanaa katika kazi moja ya fasihi. Akifafanua zaidi anaeleza kuwa, mwandishi wa kazi ya fasihi hujikuta amechanganya matini za nyimbo, semi, hadithi, hadithi ndani ya hadithi, maigizo na matumizi ya ishara katika kazi yake ya fasihi. Mtindo huo wa kuchanganya vipengele tofauti katika kazi moja ya fasihi ni kitu kilichozoeleka sana miongoni mwa wanafasihi.

Khatib (2015) katika tasnifu yake ya shahada ya uzamili, alitafiti kuhusu, *"Ufasihi Simulizi katika Riwaya za Shaabn Robert: Mifano kutoka Adili na Nduguze na Wasifu wa Siti Binti Saad."* Katika kazi yake hii mtafiti alitazama tanzu na vipera mbalimbali vya fasihi simulizi vilivyotumika na mwandishi Shaaban Robert katika utunzi wake. Wanjala (2015), *Mwingilianotanzu katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika: Mfano wa Embalu na Mwaka Kongwa*, Tasnifu ya Uzamivu. Ametafiti na kuonesha namna tanzu za fasihi simulizi zinavyoingiliana wakati wa utendaji wa tanzu moja wapo. Kwamba, ni rahisi kukuta utanzu wa ushairi ukitumika wakati wa usimulizi

wa hadithi, utumizi wa semi ndani ya hadithi n.k. Wanjala anabainisha kuwa hali hii haiko kibubusa. Ni kaida kwa fasii hii ya kiafrika, fasihi simulizi zaidi. Njogu (2017) katika mhadhara mmoja wa fasihi akifafanua kuhusu dhana ya mwingilianotanzu na mwingilianomatini anasema kwamba, “Mwingilianotanzu ni hali ya uwepo wa utanzu mmoja ndani ya tanzu nyingine ya fasihi.” Kwa mfano ushairi kuwa ndani ya riwaya.

Mwingilianomatini huwepo wakati matini kutoka tanzu mbalimbali zinakutana katika kazi moja ya fasihi ili kuendeleza maudhui. Kwa mfano, mwandishi wa riwaya au tamthiliya anaweza kurejea riwaya/tamthiliya nyingine iliyotangulia ili kujenga maudhui yake. Mtunzi anaweza hata kutumia kauli ya kiongozi au mtawala fulani katika kujenga maudhui ya kazi yako. Mf: Mandela, Nyerere, Kenyata, Museveni, Mugabe n.k Tunajifunza jambo la msingi kupitia kazi za mwandishi huyu wake kuwa mwingilianotanzu ni sehemu ya mwingilianomatini.

## 2.10 Hitimisho

Sura hii ya pili imeangazia mapitio ya kazi tangulizi kuhusu dhana ya tamthiliya kwa jumla. Tumepitia pia dhana ya mwingilianomatini katika tamthiliya. Pamoja nayo tumetalii kazi tangulizi juu ya tamthiliya za Emmanuel Mbogo. Baada ya hapo tumetazama pengo la maarifa, mkabala wa kinadharia na hatimaye nadharia ya mwingilianomatini; usuli na mihimili yake. Kuhusu nadharia ya mwingilianomatini tumeng’amua waasisi wake na mihimili yake mikuu inayoongoza nadharia hiyo. Nadharia hii ndiyo imetumika katika kueleza na kuchambua data za utafiti huu.

# SURA YA TATU

# 3.0 MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Katika sura hii tumeeleza mbinu mbalimbali tulizotumia katika kuufanya utafiti wetu. Ndani ya Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2004), istilahi mbinu inafafanuliwa kama njia ya kutekeleza jambo. Sehemu kuu tulizozitazama ni hizi zifuatazo; Mpango wa utafiti, eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, sampuli na usampulishaji, aina za data zilizokusanywa, mbinu za kukusanya data, uthibiti wa data na mbinu za kuchanganua data, usahihi na kuaminika kwa data, maadili ya utafiti hatimaye hitimisho.

## 3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu tulioufanya ulikuwa utafiti wa kimaktaba. Kwa hivyo, umefanyika hapa Dar es Salaam. Tumefanyia hapa Dar es Salaam kwa sababu, Maktaba nyingi na muhimu hapa nchini Tanzania zipo katika jiji hili. Tulitumia Maktaba kuu ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Maktaba ya Taasisi za Taaluma za Kiswahili, Makavazi ya Taasisi za Taaluma za Kiswahili (TATAKI), ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Huko maktaba tulitalii kazi mbalimbali tangulizi zinazohusiana na mada yetu ya utafiti. Kothari (1990) anasema kuwa, katika mbinu ya utafiti wa kimaktaba, utafiti hutekelezwa kwa kusoma majarida, makala, tasnifu, vitabu na machapisho mbalimbali ya kitaaluma.

Kimsingi eneo letu la utafiti lilikuwa katika tamthiliya mbili teule za Emmanuel Mbogo; *Nyerere na Safari ya Kanaani* na *Sadaka ya John Okello*. Data msingi za

utafiti huu tulizipata zote katika kazi hizi tulizoteua kuzitalii katika utafiti huu tuliofanya.

### 3.3 Usanifu wa Utafiti

Tutazamapo vyanzo vya maarifa, istilahi ya usanifu inatumika kurejelea ramani inayochorwa na mtafiti kuonyesha mpango mzima wa utafiti, kuanzia zoezi la ukusanyaji data, uchambuzi wa data mpaka uandishi wa ripoti ya utafiti. Bwelele (2016) akimrejelea Robson (2007) anaeleza kwamba, kuna aina mbalimbali za usanifu wa utafiti. Mojawapo ya usanifu huo ni uchunguzi kifani. Robson (ameshatajwa) anafafanua kuwa uchunguzi kifani ni mbinu ya mpango wa utafiti ambayo hutumika na mtafiti kuteua eneo au jambo maalum ambalo yeye analishughulikia katika utafiti wake. Katika utafiti tulioufanya tuliteua kazi mbili za tamthiliya ambazo ni *Nyerere na Safari ya Kanaani* na *Sadaka ya John Okello.* Tumeona kuwa mbinu hii ni faafu kutokana na aina ya utafiti tuliokusudia kuufanya lakini pia urahisi wake katika utumizi wa muda na gharama ndogo katika kufanikisha zoezi la utafiti.

### 3.4 Sampuli na Usampulishaji

Katika tasnia ya utafiti, Sampuli inafasiliwa kama sehemu ya watafitiwa inayoteuliwa na mtafiti kutoka kwenye populesheni kubwa iliyoandaliwa na mtafiti ili itumike katika zoezi zima la ukusanyaji wa data (Bwelele 2016). Katika utafiti tuliofanya tumetumia tamthiliya mbili za Kiswahili. Tamthiliya hizo ni *Sadaka ya John Okello* na *Nyerere na Safari ya Kanaani*. Sampuli hii imeteuliwa kutoka katika kazi nyingi za tamthiliya zilizoandikwa na Emmanuel Mbogo. Baadhi ya hizo ni; *Sundiata*, *Watoto wa Mama Ntilie*, *Fumo Liyongo*, *Nyota ya Tom Mboya*, *Wangari*

*Maathai, Malkia Bibi Titi Mohamed, Ndoto za Joseph, (tukitaja chache).* Sign (2007), anaeleza kuwa usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kundi dogo kutoka kundi kubwa la watafitiwa ili kufanya makisio ya kundi lengwa. Mwanazuoni huyu anazidi kueleza kwamba sampuli huchaguliwa kwa mbinu mbalimbali. Mfano: Usampulishaji nasibu na Usampulishaji usio nasibu. Usampulishaji ni kile kitendo cha kuchagua kitu kimoja kati ya vingi vya aina ile ile, kinachukuliwa kama mfano mzuri wa vitu hivyo kwa kuviwakilisha. Katika utafiti, usampulishaji ni kitendo cha kuteua washiriki kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa na kupata kundi lengwa litakalotumiwa katika zoezi la ukusanyaji wa data.

Watafiti mbalimbali wanaeleza aina mbalimbali za usampulishaji. Miongoni mwao ni Kothari (1990). Yeye ameainisha aina nane za usampulishaji. Katika utafiti tulioufanya tumetumia mbinu ya usampulishaji lengwa. Usampulishaji huu humpa mtafiti fursa ya kuteua sampuli anayoona kwamba itamwezesha kupata data anazozihitaji katika kukamilisha malengo ya utafiti wake. Tamthiliya teule, *Sadaka ya John Okello* na *Nyerere na Safari ya Kanaani,* zimeteulewa kwa maksudi kabisa kwa kuwa ndizo ambazo zinaweza kumpatia mtafiti data anazozihitaji.

**3.5 Aina ya Data zilizokusanywa**

Utafiti huu ulikusanya data za aina mbili; data za msingi na data za upili. Data hizi ndizo zimetumika katika kuyajibu maswali ya utafiti huu na kusaidia kukamilisha malengo yetu ya utafiti. Tulichagua kukusanya data za aina zote mbili ili tuweze kufikia malengo ya utafiti wetu kwa kiwango kikubwa. Data ambazo zimekusanywa

kutoka vyanzo mbalimbali vya maarifa na zile data mpya kabisa tulizoziibua kwa mara ya kwanza katika utafiti huu.

### 3.5.1 Data za Msingi

Hizi ni data zinazokusanywa kwa mara ya kwanza. Wakati mwingine hujulikana kama data halisi, ambazo hazijawahi kukusanywa wala kutumiwa na mtafiti mwingine yeyote kwa minajili ya utafiti kama huo unaotarajiwa kufanyika (Good, 1966). Kombo na Trumph (2006) wanaeleza kwamba data za msingi ndizo malighafi ya mtafiti. Data hizi ndizo zinazotumika kuziba pengo la utafiti liliachwa na watafiti wengine waliotangulia. Data za msingi katika utafiti huu zimekusanywa katika tamthiliya mbili teule; *Sadaka ya John Okello* na *Nyerere na Safari ya Kanaani*.

### 3.5.2 Data za Upili

Hizi ni aina ya data zilizokwisha kukusanywa tayari na watafiti mbalimbali waliotangulia. Data zilizotumiwa na watafiti hao kujibu maswali ya tafiti zao. Data za kundi hili zinaweza kupatikana katika makala, majarida, vitabu, tasnifu, tovuti na machapisho mbalimbali ambayo yanahusiana na utafiti husika. Kwa hivyo, tunaweka bayana kwamba katika utafiti huu, mtafiti amekusanya data za aina zote mbili. Data za msingi na data za upili kutoka katika matini mbalimbali katika uga wa fasihi zinazoendana ama kuhusiana na utafiti huu.

## 3.6 Mbinu za Kukusanya Data

Katika uga wa utafiti, mbinu za utafiti ni njia zinazotumiwa na mtafiti katika zoezi la ukusanyaji wa data zinazohitajika ili kuziba pengo la utafiti lililowekwa bayana katika utafiti husika. Kuna mbinu mbalimbali ambazo hutumika kukusanya data

katika utafiti. Uteuzi wa mbinu ya kukusanya data huukuliwa na aina ya data inayotakiwa kukusanywa. Mbinu za kukusanya data za msingi huwa si faafu kwenye kukusanya data fuatizi. Mbinu zinazotumika kukusanya data katika utafiti ni nyingi. Katika utafiti huu tumetumia mbinu ya usomaji makini. Tumetumia mbinu hii kwa sababu yaendana na aina ya utafiti tunaofanya pia aina ya data tunazotaka kukusanya.

### 3.6.1 Usomaji Makini

Katika utafiti tulioufanya, tulikusanya data kwa mbinu ya usomaji makini. Hii ni mbinu ya kukusanya data za msingi katika matini mbalimbali za kitaaluma kama vile kazi za fasihi mfano; riwaya, tamthiliya na ushairi na machapisho mbalimbali. Kothari (2008) anaeleza kwamba katika mbinu hii vyanzo mbalimbali vya maarifa yakiwemo machapisho hupitiwa kwa kina ili kuweza kupata data na hatimaye kufikia malengo ya utafiti. Ndiyo kusema data zote zimetoka katika machapisho mbalimbali ya kitaaluma huko maktaba. Tulitumia machapisho yanayohusiana na mada yetu tu.

Mbinu ya usomaji makini katika utafiti wetu imetumika katika kukusanya data za msingi ndani ya tamthiliya teule, *Sadaka ya John Okello* na *Nyerere na Safari ya Kanaani*. Kabla ya kuanza kukusanya data za msingi tulilazimika kuzisoma kazi hizi zaidi ya mara nne kila moja kwa siku tofauti. Hii ilitusaidia kuzielewa na kuzifahamu kwa kina. Tuzisomapo tulikuwa tukitafuta mwangwi mbalimbali wa Biblia unaojitokeza katika kazi hizo. Baada ya hapo data zilikusanywa na kuhifadhiwa katika shajara maalum. Data zilizokaribiana zimewekwa pamoja ili kurahisisha zoezi la upangaji na uchambuzi wa data. Mada hii ya *Kuchunguza Ubiblia katika Kazi za*

*Emmanuel Mbogo*, nyenzo zake kuu imekuwa Biblia na kazi teule. Kwa hivyo yote yaliyokusudiwa kuelezwa yamepatikana kwenye vitabu zaidi. Tulipendekeza kutumia mbinu hii ya usomaji makini kwa sababu ingetosheleza mahitaji ya utafiti wetu.

### 3.7 Mbinu ya Uchambuzi wa Data

Utafiti wowote huongozwa na mkabala fulani mahsusi. Waweza kuwa mkabala wa kitakwimu, kimaelezo n.k. Kwa masomo ya fasihi mkabala wa kimaelezo na mkabala usio wa kitakwimu ndiyo hutumiwa zaidi na watafiti wengi katika uga huu wa fasihi. Data za utafiti huu zitachambuliwa kwa mkabala wa kimaelezo.

#### 3.7.1 Mkabala wa Kimaelezo

John (2007) anafafanua kwamba, uchambuzi wa kimaelezo ni uchambuzi unaomruhusu mtafiti kusikiliza, au kuona au kusoma kazi ya fasihi, tamthiliya ikiwemo, kisha kuelewa maudhui yaliyomo katika kazi hiyo na vipengele vya fani pia akinuia kufanya hivyo. Katika kusoma kazi teule, mtafiti amepitia vipengele vyote vya msingi vyenye kuleteleza mwangwi wa Biblia katika kazi hizo ama vinavyoonesha ubiblia katika kazi hizo za Emmanuel Mbogo.

Vipengele hivyo vimetoka upande wa fani kwa mfano: Majina ya kazi husika, majina ya wahusika, mtindo na ploti, vitushi mbalimbali n.k. Ili kufaulu katika uchambuzi wa data katika utafiti huu tumefanya yafuatayo. Kwanza tumesoma kwa kina tamthiliya zilizoteuliwa ili kupata data za utafiti. Baada ya hapo tumezichambua data na kuzitolea maelezo yanayohusu malengo ya utafiti.

### 3.8 Usahihi na Kuaminika kwa Data

Utafiti mzuri ni ule wenye data sahihi. Usahihi wa data unaenda sambamba na utaratibu anaotumia mtafiti katika upatikanaji wa data sahihi. Bwelele (2016) akiwarejelea Cohen na wenzake (2000) anasisitiza kwamba usahihi wa data hutokana na utaratibu anaotumia mtafiti katika kuzipata data zilizo sahihi. Katika kupata data zilizo sahihi katika utafiti tunaotaraji kuufanya, tutatumia zaidi maktaba, sehemu tulivu kwa ajili ya usomaji makini ili tuweze kufikia lengo tulilolikusudia katika utafiti huu. Mkabala wa kimaelezo ndiyo tulioutumia zaidi katika uchambuzi wa data zetu.

### 3.9 Maadili ya Utafiti

Maadili ni dhana pana katika utafiti. Inaweza kurejelea kuheshimu taratibu, miiko, mila na desturi mbalimbali katika jamii. Haya ndiyo asemayo Ranjit (1999) katika kazi yake ya *Research Methodology*. Utafiti una miiko yake ambayo inapaswa kuzingatiwa. Kwa hivyo tunakiri kwamba utafiti huu umezingatia na kufuata maadili yote ya msingi yanayohitajika kuzingatiwa kila zoezi la utafiti linapofanyika. Tumezingatia zaidi uaminifu katika mapitio ya tafiti mbalimbali za wanazuoni tuliowarejelea katika utafiti huu na kuepuka upotoshaji wa data katika uchanganuzi wake na hata matokeo ya utafiti.

### 3.10 Hitimisho

Katika sura hii ya tatu tumeonyesha mambo muhimu yanayohusu utafiti. Tumezungumza kuhusu eneo la utafiti na usanifu wa utafiti. Tumetazama pia vipengele vya sampuli na usampulishaji, aina za data zilizokusanywa:data za msingi

na data za upili, mbinu zilizotumika kukusanya data;usomaji makini, mbinu za uchambuzi wa data:mkabala wa kimaelezo na kisha tukatazama usahihi na kuaminika kwa data na hatimaye maadili ya utafiti.

# SURA YA NNE

# 4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ZA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Katika sura hii ya nne tumechambua na kujadili data kutoka katika vyanzo mbalimbali vya data zinazohusu utafiti huu. Malengo mahsusi yote mawili yamechambuliwa sambamba, kwanza kubainisha ubiblia ulivyojitokeza na kisha kueleza sababu ya utokezaji wa ubiblia huo. Sehemu ya kwanza ya sura hii imeeleza kuhusu mtunzi, sehemu ya pili hadi ya nne inawasilisha, kuchambua na kutoa matokeo ya data za utafiti huu na hatimaye hitimisho katika sehemu ya tano.

## 4.2 Ubiblia na Sababu za Utokezaji wake katika *Nyerere na Safari ya Kanaani* na *Sadaka ya John Okello*

Utafiti huu uliongozwa na malengo mahsusi mawili. Lengo mahsusi la kwanza lilikuwa kubainisha vipengele vya kibiblia katika tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani* na *Sadaka ya John Okello.* Lengo mahsusi la pili ilikuwa kueleza sababu ya utokezaji wa vingele vya kibiblia katika kazi teule za Emmanuel Mbogo. Malengo yote mawili yameunganishwa katika uchambuzi kwa sababu yanahusiana kimantiki. Malengo mahsusi haya yanakamilisha lengo kuu moja la utafiti ambalo ni kuchunguza ubiblia katika tamthiliya za Emmanuel Mbogo. Katika uchambuzi, kwanza tutabainisha ubiblia uliojitokeza katika kazi husika kisha tutaeleza sababu ya kujitokeza kwa ubiblia huo katika kazi husika. Sifa moja inayoonyesha ubiblia itatazamwa kutoka katika kazi teule zote mbili kabla ya kuhamia sifa nyingine. Ili kufikia malengo haya, utafiti huu ulitumia mbinu ya usomaji makini kwa kusoma,

kuchunguza tamthiliya hizo. Nadharia tuliyoitumia kuchambua data za utafiti ni nadharia ya mwingilianomatini. Utafiti huu ulibaini kuwa utunzi wa tamthiliya za *Nyerere na Safari ya Kanaani* na *Sadaka ya John Okello* ni matokeo na athari ya mafundisho na mapokeo ya Ukristo ambayo yalimuathiri mtunzi na kuyatumia mapokeo hayo kuzalisha tamthiliya hizo. Sambamba na hilo utafiti huu ulibaini kuwepo na mwingilianomatini wa Biblia katika kazi hizi za fasihi ambapo kuna matini zilizotumika katika Biblia zinajitokeza katika tamthiliya hizi. Kimsingi, sehemu hii inabainisha matumizi ya mwingilianomatini kwa kubainisha matini za Biblia zilizojitokeza katika tamthiliya za *Nyerere na Safari ya Kanaani* na *Sadaka ya John Okello*. Kwa kutumia mbinu ya usomaji makini inayojumuisha mapitio ya maandiko, mtafiti alibainisha matini za Biblia zifuatazo katika jedwali hapa chini. Matini hizo zimetumika kufanya uchambuzi katika tamthiliya zote mbili zilizoteuliwa.

**Jedwali namba 4.1: Matini za Biblia zilizotumika katika Utunzi wa *Nyerere na Safari ya Kanaani* na *Sadaka ya John Okello***

| Na. | Aina ya Matini ya Biblia iliyojitokeza katika kazi teule |
|---|---|
| 1. | Jina la Kitabu |
| 2. | Hadithi ya Biblia |
| 3. | Wahusika wa Biblia |
| 4. | Nukuu za Biblia |
| 5. | Ushairi wa Biblia/Zaburi |

### 4.2.1 Jina la Kitabu

Hili ni jina ambalo hubeba na kutambulisha kazi yoyote ya fasihi. Dhana hii inafafanuliwa kwa namna mbalimbali na wanazuoni katika uga wa fasihi. Miongoni mwao ni Lema (2010). Yeye anaeleza kwamba jina la kitabu ni kichwa cha habari

kinachobeba kazi nzima ya fasihi; riwaya, ushairi ama tamthiliya. Jina hili linapaswa kudokeza kiini cha jambo kuu linalosemwa na kujadiliwa katika kazi husika. Ndiyo kusema, hueleza lengo kuu la kazi ya fasihi kwa muhtasari. Mtu asomapo tu ama akutanapo tu na jina hilo, ujumbe fulani wasikika mbongoni mwake. Tutachambua jina la tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani* na hatimaye kumaliza na tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* ili kubainisha ubiblia unaojitokeza humo.

*Nyerere na Safari ya Kanaani* ndilo jina la moja ya tamthiliya tuliyoitafiti. Mtafiti alipokuwa maktaba aling'amua kwamba jina la tamthiliya hii ni tokeo la mapokeo ya kikristo aliyonayo mwandishi wa kazi hii Emmanuel Mbogo. Jina hili linanasibishwa na historia ya taifa la Israel lililokuwa utumwani Misri kwa zaidi ya miaka mia nne. Wakati wa ukombozi ulipowadia, wakatolewa utumwani na kuongozwa na Nabii Musa ili warudi kwao, Israel (Kanaani inayosemwa na Emmanuel Mbogo).

Kwa mujibu wa Julia Kristeva (1980) katika ufafanuzi wake juu ya nadharia ya mwingilianomatini, kazi yoyote ya fasihi ni tokeo la kazi ama matini nyingine zilizopata kuwepo hapo awali kabla ya kazi hiyo husika. Kwa hivyo hata mbinu ya uteuzi wa jina la kitabu hutokana na muathiriano wa kazi hizo za fasihi zilizotangulia mapema kabla ya hiyo inayotungwa na msanii wakati huo wa sasa. Utafiti ulibaini kwamba, jina la kitabu hiki linaposikika tu masikioni mwa watu, basi kuna mwangwi wa Biblia unaosikika katika mbongo za watu, hasa wa mapokeo ya kikristo juu ya safari ya wana wa Israel kutoka utumwani Misri kwenda nchi ya maziwa na asali Kanaani, aliyowaahidia Mola wao kuwa atawapa kupitia manabii wa awali akina Abrahamuu. Kwenye Biblia habari kuhusu safari ya Waisrael kwenda Kanaani

inapatikana katika kitabu cha *Kutoka*. Jina la Kanaani limetamkwa katika, Kutoka 3:15-17.

> Tena Mungu akamwambia Musa, waambie wana wa Israel maneno haya, Bwana, Mungu wa baba zenu, Mungu wa Abrahamu, Mungu wa Isaka, Mungu wa Yakobo, amenituma kwenu; hili ndilo jina langu hata milele, nalo ni kumbukumbu lango hata vizazi vyote. Enenda ukawakusanye wazee wa Israel pamoja, ukawaambie, Bwana, Mungu wa Baba zenu, Mungu wa Abrahamuu, Mungu wa Isaka, Mungu wa Yakobo, amenitokea, akaniambia, Hakika nimewajilieani, tena nimeyaona mnayotendewa huko Misri; Nami nimesema, nitawapandisha kutoka Misri na kuwaingiza katika nchi ya Mkanaani, na Mhiti, na Mwamori, na Mperizi, na Mhivi, na Myebusi, nchi ijaayo maziwa na asali.

Chanzo: Data za Utafiti katika Biblia Takatifu-Kutoka 3:15-17.

Kwa hivyo, jina la kitabu hiki kwa mujibu wa nadharia ya mwingilianomatini hakika ni tokeo la athari ya safari hiyo ya wana wa Israel kutoka utumwani kwenda Kanaani, nchi aliyowaahidia Mungu kuwapa. Nchi hiyo inanasibishwa na nchi ya raha, iliyojaa maziwa na asali. Hakuna tabu wala masumbuko huko. Kwa msingi wa nadharia ya mwingilianomatini, mtunzi ameinasibisha safari hii ya kanaani na safari ya Tanzania kuelekea maendeleo yake chini ya utawala wa wazawa wenyewe mapema baada ya kupata uhuru kutoka kwa wakoloni. Emmanuel Mbogo ameakisi ubiblia katika uteuzi wa jina la kazi yake hii. *Sadaka ya John Okello* ndilo jina la kazi nyingine hii fasihi tuliyoitafiti katika utafiti huu kupitia nadharia ya mwingilianomatini. Tumekwisha zungumza huko juu kwamba jina la kitabu hudokeza kwa muhtasari dhamira kuu ya kazi ya fasihi. Pengine tutazame kwanza namna dhana ya sadaka inavyotazamwa kisha tuendelee na upembuzi wa jina hili ili

kubaini mwangwi wa Biblia unavyojitokeza. Jacob na Makaya (2016) wanasema, Sadaka ni neno ambalo mara nyingi sana limemaanisha kitu kilichotolewa bure mahali. Tusikiapo mtu ametoa sadaka tunaelewa kuwa mtu huyo ametoa kitu hicho bure pasina kutaraji mrejesho au malipo kwa huyo anayemtolea. Wachungaji hawa wanaeleza kwamba kutoa sadaka kunanasibishwa na ishara ya upendo, kwamba kama mtu hana moyo wa upendo hawezi kutoa sadaka. Ufafanuzi huu uliotolewa ni kweli na utatusaidia katika kupambanua dhamira kuu ya kitabu iliyojificha kwenye jina la kitabu.

Makange (2012), "Sadaka ni zawadi inayotolewa kwa Mungu, kwa kusudi la kuonyesha upendo, heshima na uthamani wa Mungu katika maisha ya mtu. Katika Biblia Takatifu hili linathibitishwa kutoka Ezra 2: 68-69. Maneno ya Mungu yanasema hivi;

> "Na baadhi ya wakuu wa mbari za baba zao, hapo walipofikilia nyumba ya Bwana, iliyoko Yerusalem, walitoa mali kwa ukarimu kwa ajili ya nyumba ya Mungu, ili kusimamisha mahali pake; wakatoa kadri walivyoweza, na kutia katika hazina ya kazi hiyo, darkoni za dhahabu sitini na moja elfu, na nane za fedha elfu tano, na mavazi mia ya makuhani."

Chanzo: Data za Utafiti katika Biblia Takatifu, Ezra 2:68-69.

Katika kitabu cha Biblia sadaka ni tendo linalofanywa kwa namna ya kutafsiri moyo kwa matendo, kuonyesha kwamba unampenda Mungu. Kutoa sadaka ni sehemu ya kukamilisha ibada ya mtoaji mbele za Mwenyezi Mungu. Vitabu vya dini vinawakumbusha waamini kutoa sadaka kwa hiari yao wenyewe pasina kulazimishwa na mtu. Aina na kiwango cha sadaka mtu anayotoa ndicho kinadhihirisha mtu anampenda Mungu kiasi gani. Waaidha mwamini anaruhusiwa

kutoa sadaka kwa njia ya kuwasaidia wengine, wahitaji na wasiojiweza. Kumsaidia mhitaji chakula ni sadaka kwa Mwenyezi Mungu. Kusaidia mavazi au huduma za matibabu zote hizo katika mafundisho kwenye vitabu vya imani, Biblia ikiwemo ni sehemu ya sadaka. Katika utafiti wetu tuliofanya kwa kuegemea nadharia ya mwingilianomatini, katika mhimili mmojawapo, Bhaktin anasema kwamba kazi yoyote ya fasihi ni tokeo la kazi nyingine tangulizi iliyopata kuwepo kabla ya hiyo mpya tulibaini kuwepo kwa mwingilianomatini baina ya matini hizi mbili; Biblia na tamthiliya tuliyotafiti. Neno ‘sadaka’ liliteuliwa kuwakilisha dhana hiyo ya utoaji wa kitu cha thamani bure.

Katika kazi teule mtoaji wa sadaka hii ni mhusika mkuu, John Okello. John Okello alipambana kufa na kupona hata kuweka maisha yake hatarini kwa lengo la kuitetea na kuikomboa Zanzibar kwa kuongoza mapinduzi. Alisimamia mpango mzima wa kuikomboa jamii hiyo lakini mapinduzi yafanikiwapo na mgeni kuachia madaraka, Okello alifukuzwa na kusahaulika kama alitoa mchango wowote katika zoezi hilo. Pengine ndiyo maana mwandishi ameiita kazi yake *Sadaka ya John Okello*, kwamba sadaka ni kitu unachotoa bure na hautazamiwi kurudishiwa. Unatoa kisha unasonga mbele bila kugeuka nyuma. Mtunzi anasema haya katika onyesho la kumi uk.55, jinsi Okello anavyogeukwa.

**ZIMWI 1**: John Okello, wewe nani?

**ZIMWI 2**: Okello! Okello, umefuata nini visiwani?
Hapa visiwani hakuna Msalaba
Hapa Zanzibar tunatazama Kibla
Hatutazami Golgota

Chanzo: Data za utafiti katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* (uk. 55).

Kimsingi, uteuzi wa majina ya vitabu katika tamthiliya hizi zote mbili kwa kutumia nadharia ya mwingilianomatini tumebaini kuwa umetokana na athari za Biblia kwa mtunzi. Mapokeo ya kikristo ndiyo sababu ya kutokea kwa majina ya tamthiliya hizi. Ni ukweli usiopingika kwamba Emmanuel Mbogo ameegema zaidi katika mkondo wa kibiblia alipoteua majina ya kazi zake. Jina la *Nyerere na Safari ya Kanaani* na *Sadaka ya John Okello* ni chipukizi la mapokeo hayo ya kibiblia aliyokulia mwandishi Emmanuel Mbogo. Kwa hivyo, ubiblia umedhihirika kupitia majina ya kazi zake.

### 4.2.2 Hadithi ya Biblia

Wanazuoni katika uga wa fasihi wanaifafanua dhana ya hadithi kwa namna mbalimbali. Ndungo na Wangari (1991) wanafafanua dhana ya hadithi hivi, "Hadithi ni masimulizi ya kinathari, yaani yasiyo ya kishairi." Wanaendelea kusisitiza kwamba, hadithi huwa na wahusika ambao huzungumza na matendo yanayotendwa na wahusika hao huleta mtiririko wa matukio unaokamilisha hadithi hiyo. Matukio katika hadithi yanaweza kuwa ya kweli au ya kubuni. Fafanuzi hii imetufaa kuelewa maana ya hadithi kabla hatujauendea uchambuzi wetu. Vilevile mwanafasihi Msokile (1992) anasema, "Hadithi ni kazi ya sanaa inayotumia lugha." Tulipokuwa tukimsoma mwanazuoni huyu tulibaini kwamba, hadithi yaweza kuwa ya masimulizi ya kubuni ama ya kweli yaliyo katika mfumo wa nathari. Katika andiko la mwanazuoni huyu tuling'amua kuwa hadithi ni kazi ya mtu yenye mwigo wa kiyakinifu uliofungamana na wakati, mazingira na mfumo wa jamii. Dai hili ni sahihi kwani hadithi hutokana na jamii na mazingira fulani mahsusi. TUKI (2014), wanafasili dhana ya hadithi kwamba ni habari ya mambo yaliyotukia, mtungo wa

habari, kisa, ngano, masimulizi, hekaya. Wanazuoni hawa kutoka taasisi ya taaluma za Kiswahili (TATAKI) wakati huo TUKI wanaeleza jambo la msingi kuihusu hadithi. Kuwa ni habari ya mambo yaliyotukia. Tutazamapo kwa makini humu ndani ya fasili hii dhana ya ukweli wa habari hiyo inajitokeza zaidi. Kwamba jambo linalosimuliwa huwa limetukia kabla, huko nyuma. Katika *Nyerere na Safari ya Kanaani*, utafiti huu ulibaini kuwa mtunzi ametumia matini ya hadithi ya Biblia kuijenga kazi yake. Tamthiliya hii ni tokeo la masimulizi yahusuyo wana wa Israel, kama inavyoelezwa kwenye Biblia katika agano la kale.

Hadithi inayosimuliwa kuhusu taifa hilo la Israel lililokuwa utumwani huko nchini Misri kwa muda wa miaka mia nne. Baada ya miaka hiyo ya utumwa Mungu alimsimamisha nabii miongoni mwao aitwaye Musa ili awaongoze na kuwatoa katika nchi ya utumwa na kuwaleka Kanaani, kwa sasa Israel. Kristeva (keshatajwa) anabainisha kuwa kazi za fasihi huingiliana na kuathiriana kwa namna mbalimbali. Pengine ili tutazame na kuona waziwazi mwingiliano huu wa Biblia katika tamthiliya hii basi tuisome hadithi hii iliyoandikwa kuhusu Wana wa Israel, namna walivyotoka nchini mwao na kwenda utumwani na mwisho kabisa namna walivyorudi katika nchi yao. Masimulizi hayo yanadai hivi;

Hapo mwanzo Mungu aliumba mbingu na nchi. Akamuumba mtu akamweka katika nchi hiyo, akakubaliana naye kuwa ailinde, aitunze, tena aweze kuimiliki. Mtu huyo akakiuka makubaliano yake na Mungu ambayo walikubaliana. Mtu huyo alifukuzwa na kuondolewa katika nchi ile aliyokuwa amewekwa ndani yake ili aweze kuitunza. Baada ya miaka elfu moja ya mtu huyo kufukuzwa kutoka katika nchi ile Mungu alimtafuta mtu miongoni mwa wanadamu atakayemtumia kutimiza kusudi lake.

Katika mpango huo akampata mtu ambaye aliitwa Abramu, ambaye baadaye alimbadilisha jina kutoka Abramu maana yake Kuhani wa Mungu akawa Abrahamu, baba wa Mataifa, Kuhani wa Mungu aliye hai. Ilikuwa imepita miaka elfu moja mpango wa kwanza uliposhindwa wa kumpata mtu huyo. Abrahamu alipewa masharti ambayo akiyakubali ndipo akubaliwe kutumiwa na Mungu. Tunasoma katika kitabu cha kiitwacho Mwanzo katika Biblia hivi;

> BWANA akamwambia Abrahamu, Toka wewe katika nchi yako na jamaa zako, na nyumba ya baba yako uende mpaka nchi nitakayo kuonesha, nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki, na kulikuza jina lako nawe uwe baraka, Nami nitawabariki wakubarikio, naye akulaaniye nitamlaani, na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa.
>
> Chanzo: Data za Utafiti katika Biblia Takatifu, Mwanzo 12:1-3.

Mungu alimuahidi huyo mtu mambo makuu matano ikiwa atakubali kufanya kama anavyomwagiza Kwanza: Atampa nchi, Pili: Atamfanya kuwa Taifa kubwa, Tatu: Atamfanya kuwa Baraka, Nne: Jamaa zote za dunia watabarikiwa kupitia yeye, Tano: Atawabariki wambarikio na kumlaani Yule Atakaye mlaani. Mtu huyo alikubali masharti hayo yote ambayo Mungu alimpa Mwanzo 17:6-7. "Nitakufanya uwe na uzao mwingi sana, nami nitakufanya kuwa taifa, na wafalme watatoka kwako. Agano langu nitalifanya kuwa imara kati ya mimi na wewe, na uzao wako baada yako na vizazi vyao kuwa agano la milele, kwamba nitakuwa Mungu kwako na kwa uzao wako baada yako.Nami nitakupa wewe na uzao wako baada ya yako nchi hii unayo ikaa ugeni, nchi yote ya Kanaani, kuwa milki ya milele, nami nitakuwa Mungu wao." Mungu alimpa Abrahamu nchi ya Kanaani kuwa milki yake, yeye na uzao wake. Kanaani lilikuwa ni jina la nchi ambayo leo hii inaitwa Israel, kwa sasa.

Masimulizi kwenye Biblia yanaendelea kusema baadaye taifa la Israel ni masalia ya Mzee Abrahamu ambaye ni babu kwa mjukuu wake Yakobo aliyeitwa Israel baadaye. Mapokeo ya kikristo yanasema kwamba watu hawa walikaa huko utumwani, Misri muda wa miaka mia nne walipoenda kwa sababu ya njaa hadi hapo Mola wao alipoamua kuwakomboa kupitia Nabii Musa ili warudi kwao Israel, walikokuwa awali kabla ya kwenda utumwani.

Safari yao kurejea kwao iliwachukua muda wa miaka arobaini kufika nchini mwao. Katika miaka hiyo arobaini Mungu akafanya agano pamoja nao ambalo liliwatofautisha na mataifa mengineyo. Mungu akawapa amri kumi ambazo zingewaongoza katika maisha yao. Israel waliingia Kanaani chini ya Yoshua. Nabii Musa alifia njiani, wala hakuingia nchi ya ahadi ambayo Mungu aliwaahidia wana wa Israel. Masimulizi kuhusu nchi hii yanapatikana katika vitabu vya awali katika Biblia Takatifu ya Kikristo. Kitabu cha Mwanzo, Kitabu cha Kutoka, Mambo ya Walawi, Hesabu na Kumbukumbu la Torati. Imebainika kwamba vitabu hivi vyote vitano vya mwanzo katika Biblia viliandikwa na Nabii Musa.

Wamitila (2003) na Senkoro (2011) wanasema kuwa msingi mojawapo wa nadharia ya mwingilianomatini iliyoasisiwa na Mikhail Bakhtin unasema kuwa, mtunzi huchota matini ya kazi moja ya fasihi na kuihamisha katika matini nyingine ya fasihi. Utafiti ulibaini kwamba mtunzi wa tamthiliya hii aliathiriwa na masimulizi haya kuhusu wana wa Israel. Nadharia hii ilitusaidia kubaini kuwa matini ya Biblia ilihamishwa na kuingizwa katika matini mpya ya tamthiliya ya Kiswahili lakini wakati huu ikizungumzia jamii ya kitanzania na kiongozi wao Mwalimu Julius Kambarage Nyerere anayenasibishwa na Nabii Musa aliyewaongoza wana wa Israel.

Utafiti umebaini kuwa Nyerere amenasibishwa na Musa huku taifa la Tanzania likinasibishwa na taifa la Israel. Kristeva (1980) akiendeleza mawazo ya mwasisi wa nadharia hii Mikhail Bakhtin, ambayo ilijulikana hapo kwanza kama nadharia ya usemezano anasema kwamba, mbinu ya uteuzi wa matini hutokana na muathiriano wa kazi za fasihi zilizotangulia na kusaidia katika uanishaji wa kazi za baadaye. Kristeva anaifafanua dhana hii kama jumla ya maarifa na mbinu zinazoifanya matini kuwa na maana. Maana ya matini inaangaliwa kama inayoitegemea matini nyingine.

Kwa hivyo utafiti umebaini kuwa kuna mwingiliano au mwangwi wa Biblia kati ya hadithi hiyo ya wana wa Israel, ya kutoka utumwani Misri na tamthiliya hii inayoeleza mwanzo wa safari ya taifa la kitanzania katika kujitawala na kujitafutia maendeleo ya kweli baada ya kutawaliwa na kunyonywa kwa muda mrefu na serikali za kikoloni. Kwa mujibu wa nadharia ya mwingilianomatini tumeona uhusiano uliopo baina ya hadithi hiyo ya wana wa Israel na tamthiliya hii. Pia katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello*, utafiti huu ulibaini kwamba kisa cha tamthiliya hii kinaendana na kisa kimojawapo kwenye Biblia, cha ujio wa Yesu Kristo hapa ulimwenguni.

Biblia inasema mtume huyu alikuja duniani kuwakomboa wanadamu na dhambi zao. Lakini wanadamu hawakumpokea badala yake wakamsulubisha, wakamtesa hadi kufa. Mapokeo ya ukristo yanaendelea kudai kuwa mtume huyu alisalitiwa na mmoja wa wanafunzi wake aitwaye Yuda Iskariote. Bila hatia yoyote alihukumiwa kifo na mamlaka za kifalme. Hadithi hii ya Biblia imechangia kwa namna moja ama nyingine utunzi wa kazi hii ya *Sadaka ya John Okello*. Mtume huyu Yesu katika Biblia pamoja na kung'amua kwamba hao wanadamu anaotaka kuwakomboa kutoka

kwenye utumwa wa dhambi watamkataa na kumuua bado aliendelea na mpango wake wa ukombozi. Mtume huyu alikuwa tayari kufanyiwa jambo lolote lakini tu atimize malengo ya baba yake aliyemtuma humu ulimwenguni.

Tutazame hapa;

> Yesu akawaambia, chakula changu ndiyo hiki, nikayatende mapenziyake aliyenipeleka, nikaimalize kazi yake.

Chanzo: Data za Utafiti katika Biblia-Yohana 4:34

Mwangwi wa simulizi hii unatokea pia katika tamthiliya hii teule tuliyoitafiti. Mhusika mkuu, John Okello pamoja na kutambua kwamba baada ya mapinduzi atasalitiwa na kufukuzwa lakini bado anaendelea na mpango huo. Aliuona uovu utakaotendwa juu yake lakini hakukata tamaa wala kuvunjika moyo. Alikuwa tayari kuhakikisha lile alilolikusudia linatimia. Okello anasema;

**OKELLO**: Kweli mimi ni Mganda kutoka wilaya ya Lang'o, lakini Mungu alinituma nije kuwakomboa ndugu zangu wa visiwani … Na baada ya ukombozi, tukishamng'oa Sultan

Jamshid, Wazanzibar watanigeuka. Watanisaliti. Watanigeuza kioja. Kisonoko. Kijibwa chenye mkuje kasoro mkia…"

Chanzo: Data za utafiti katika *Sadaka ya John Okello* (Uk29)

Nadharia ya mwingilianomatini iliyoasisiwa na Mikhail Bakhtin ina mhimili usemao kuwa hakuna kazi halisi, nyingi huwa ni mageuzi ya kazi nyingine za kale alizopata kukutana nazo mtunzi kabla ya kazi husika. Tusomapo kazi hizi mbili, Biblia na tamthiliya hii tunaona masimulizi kuingiliana. Mapokeo yanayoeleza habari za kusalitiwa, kuteswa na kutendwa kwa mtume Yesu ndizo zinazojitokeza katika tamthiliya hii ya John Okello. Mtu asomapo kazi hii mwangwi wa Biblia unasikika katika masikio yake anakumbuka ama kurejea simulizi hii ambayo imeshawahi

kuelezwa katika Biblia. Sambamba na hiyo kuna kisa kuhusu usaliti. Wahusika wote wawili, Yesu kutoka kwenye Biblia na John Okello kutoka kwenye tamthiliya hii walitabiri kuhusu kusalitiwa kwao. Kila mmoja alieleza kwamba atasalitiwa hapo baadaye na bado akaendelea na mpango aliokuwa amekusudia. Wote waliadhimia kusonga mbele. Hakuna mmoja miongoni mwao aliyekata tama pamoja na kujua kwamba hapo baadaye atafanyiwa vibaya. Katika Biblia tunapata habari hizi za Yesu,

> Walakini tazama, mkono wake yeye anayenisaliti upo hapa pamoja nami mezani; kwa kuwa Mwana wa Adam aenda zake kama alivyo kusudiwa, lakini ole wake mtu yule amsalitiye.

Chanzo: Data za utafiti katika *Biblia Takatifu*-Luka 22:21

Katika Luka 18:31-33 tunaona kwamba Mtume Yesu anawajuza wanafunzi kuwa wanapanda kwenda Yerusalem na kwamba mambo yote yaliyotabiriwa kumuhusu yatatimia huko. Ndiyo hiki kinachosemwa kuwa pamoja na Yesu kufahamu kinachotukia mbele bado aliendelea na safari. John Okello naye anatabiri kuhusu masaibu yatakayomkuta. Alitabiri na kunena hayo wakati yuko kwenye kambi ya maandalizi ya mapinduzi. Azungumzapo na wafuasi wake anatabiri hivi;

> **OKELLO***:* "…Na baada ya ukombozi, tukishamng'oa Sultan Jamshid, Wazanzibar watanigeuka. Watanisaliti. Watanigeuza kioja. Kisonoko. Kijibwa chenye mkuje kasoro mkia…"

Chanzo: Data za utafiti katika *Sadaka ya John Okello* (Uk 29)

Nadharia ya mwingilianomatini inatusaidia kubainisha matini za Biblia zilizomo humu kwenye kazi hii ya Fasihi. Kisa kinamchotea na kusibu mtume Yesu ndicho kinachotokea na kumsibu Field Marshall John Okello. Mtume aliyatoa maisha yake

kama sadaka kwa Mwenyezi Mungu ili awakomboe wanadamu kutoka kwenye dhambi (inavyobainishwa kwenye Biblia) na John Okello anayatoa maisha yake kama sadaka ili kuwakomboa wazanzibar kutoka kwenye uhuru wa uongo walioachiwa na mkoloni mwingireza kwa kuwaachia wageni, waarabu badala ya watu weusi. Mwingilianomatini unasisitiza pia kuwa hata maana za matini hukamilishana. Hapana shaka kuwa aliyewahi kukutana na masimulizi haya kumhusu mtume Yesu anaweza kung'amua kwa wepesi simulizi hii inayotolewa katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello*.

Kwa jumla mwangwi wa kibiblia unaonekana katika tamthiliya zote hizi mbili tulizozitafiti. Mtunzi amejenga visa vyake kupitia simulizi zilizomo kwenye Biblia. *Nyerere na Safari ya Kanaani* ni tokeo la masimulizi kulihusu taifa la Israel kukombolewa kutoka utumwani na kurudi kwao Israel ama Kanaani kama inavyobainishwa kwenye Biblia. *Sadaka ya John Okello* imejengwa kutoka kwenye kisakale cha mateso ya mtume Yesu Kristo katika mapokeo ya kikristo yanayopatikana kwenye kitabu chao kitukufu, Biblia.

### 4.2.3 Wahusika wa Biblia

Wanazuoni mbalimbali wamefafanua na kueleza dhana ya wahusika katika uga wa fasihi. Miongoni mwao ni Wamitila (2002), anafafanua dhana ya wahusika kuwa ni binadamu wanaopatikana katika kazi ya fasihi na ambao wana sifa za kimaadili, kitabia, kiitikadi na kifalsafa ambazo hutambulishwa na wanayoyasema (mazungumzo) na wanayoyatenda (matendo). Maelezo ya mwanazuoni huyu yanatusaidia kuelewa dhana hii ya wahusika kuwa ni binadamu katika kazi ya fasihi, na kwamba wahusika hawa hutumiwa na mtunzi kwa malengo mahsusi ili kufikisha

kusudi alilonalo kwa jamii, hadhira husika. Mwenda (2004) anaeleza kuwa mhusika katika fasihi ni kiumbe hadithini kilichobuniwa na msanii ili kuendeleza hoja na maudhui yake katika kazi yake. Tunajifunza kwa Mwenda kuwa wahusika wote katika kazi ya fasihi ni zao la ubunifu wa msanii, kwamba msanii huwabuni hao na kuwabebesha ujumbe au dhamira ambayo ameikusudia jamii iipate. Mlaga (2010) anasema kwamba wahusika katika uga wa fasihi hutazamwa zaidi katika makundi mawili, wahusika wakuu na wahusika wasaidizi. Wahusika wakuu ni wale wanaobeba dhamira kuu katika kazi ya fasihi. Hawa ndiyo vipaza sauti vya mwandishi. Wahusika wasaidizi ni wanaojitokeza katika sehemu chache chache. Hutumiwa kama sehemu tu ya kukamilisha kazi hiyo. Tunaungana na Mlaga katika dai lake kuwa msanii huwatumia wahusika katika kukuza dhamira. Tunaona kuwa wahakiki wanawagawa wahusika hawa wasaidizi katika aina mbalimbali. Aina hizo ni, wahusika bapa, wahusika mviringo, wahusika jumui, wahusika foili, wahusika vikaragosi na wahusika vinyago.

Kwa jumla wahusika ni viumbe hai au visivyo na uhai ambavyo vinawakilisha watendaji halisi katika maisha ya kila uchao ya jamii husika. Wahusika hutumika kueleza hali halisi ya maisha katika jamii. Msanii hutumia wahusika mbalimbali katika kuijenga kazi na kuifanya kazi yake izidi kusonga mbele. Mhusika hupewa maneno, dhana na hulka ambazo ni muhimu katika kujenga kisa kizima cha kazi husika ya fasihi, kujenga dhamira na maudhui kwa jumla. Tunaposoma tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani*, kwa kuzingatia mwega wa nadharia ya mwingilianomatini yake Mikhail Bakhtin na kuendelezwa na Julia Kristeva utafiti huu ulibaini kwamba wapo wahusika mbalimbali waliotumika katika tamthiliya hii

wanaotoa taswira na mwangwi wa Biblia katika macho ya msomaji na masikio ya msikilizaji. Mtunzi wa kazi hii, Emmanuel Mbogo amemchora mhusika mkuu Nyerere, kiongozi wa kwanza wa taifa la Tanzania sawa na Nabii Musa aliyekabidhiwa taifa la Mungu, Izrael aliongoze liende kwao Kanaani kutoka utumwani Misri. Tutazame ithibati, katika Onyesho la Kwanza la Tamthiliya hii, wanafunzi wa chuo kikuu cha Dar es Salaam wakizungumza.

**SALEHE**: Hapana! Siyo Hambiliki! Anaitwa "Nabii Musa" (wote wanacheka)

**MARTIN**: Kama sera zenyewe ndiyo hizi, sidhani kama huyu Musa wetu atatuvusha Bahari ya Sham.

**DAMARIS**: Ama kutufikisha Kanaani; nchi nzuri ya kupendeza. Nchi ya maziwa na asali.

Huko anasema Julius-hapana- Musa! Musa anasema; huko Kanaani tutarithi

Maghotofa usiyoyajenga, visima tusivyovichimba, mashamba ya zabibu na makomamanga; …"

Chanzo: Data za Utafiti kutoka Tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani (*uk3)

Wanafunzi hawa wakiwa katika mazungumzo juu ya mustakabali wa sera waliyotangaziwa ya kujiunga na jeshi la kujenga taifa (JKT) mara tu wamalizapo masomo yao na mshahara wao kukatwa asilimia sitini wanamnasibisha Nyerere na Musa anayepatikana katika kitabu cha Kutoka, kwenye Biblia. Kwa hivyo humu ndani aliyechorwa na kuvikwa uhusika wa nabii Musa ni Nyerere peke yake. Ndivyo jamii ilivyokuwa ikimtazama, wanafunzi na baraza lake la mawaziri wameonyesha

hilo wakiwa katika majadiliano mbalimbali kumuhusu. Tutazame mifano kutoka *Nyerere na Safari ya Kanaani*.

> **DAMARIS**: Yule ni Musa bwana! Anataka kutupeleka Kanaani, nchi ya maziwa na asali.
>
> **KAMBONA**: Ndiyo maana watu mitaani wanakuita Nabii Musa. Unataka kutupeleka Kanaani kunako nchi ya asali na maziwa. (Uk.5)

Mtunzi pia anamchora Nyerere kukubali na kuifurahia taswira anayovikwa kuhusu Nabii Musa akiwa kwenye mazungumzo na waziri wake Kambona. Wanasema haya wakiwa faragha;

> **NYERERE**: (anacheka kidogo) Jina la Musa mimi silikatai. Mimi Mkatoliki bwana Oscar. Kama wangeniita Goliati! (anacheka) Hawa watu wangeniita Goliati, ningekasirika sana. Lakini "Musa! Musa!" Musa ni sawa! Nina maono ya kuwapeleka Kanaani kwenye nchi ya asali na maziwa.
>
> **KAMBONA**: Tatizo la Musa wa Exodus ni kuwa, yeye mwenyewe hakufika nchi ya Kanaani…

Chanzo: Data za Utafiti kutoka Tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani* (uk 14).

Nadharia ya mwingilianomatini ina mhimili usemao kwamba, matini yoyote ile ni mabadiliko ya mpangilio wa matini nyingi tangulizi. Charney na Plotell (1978) wanashadidia hilo, kwamba matini ya kifasihi si zao la mwandishi pekee. Wao wanasisitiza kuwa matini nyingi ni tokeo ama zao la matini tangulizi alizowahi kukutana nazo mtunzi wa kazi ya fasihi kabla. Tutazamapo tamthiliya hii ya *Nyerere na Safari ya Kanaani* mhimili huu unabainika wazi. Tunaona kwamba kazi hii na

wahusika waliotumika kuijenga ni tokeo la matini inayopatikana kwenye Biblia. Kisa kimefanana na wahusika wamenasibishwa na wale waliomo kwenye Biblia. Nyerere kufananishwa na Musa wa kitabu cha KUTOKA katika Biblia ndiyo usadifu wenyewe wa mwingiliano huu. Nyerere alitaka kuiepeleka Tanzania katika nchi ya maziwa na asali, Kanaani kwa kutumia sera ya Ujamaa na Kujitegemea. Sambamba na huyo amechorwa mhusika mwingine mwishoni mwa mchezo kwa jina la Yoshua. Yoshua alikuwa msaidizi maalumu wa Musa. Yeye peke yake alifuatana naye alipokwea mlima, ambapo Musa alikutana na Mungu katika wingu, lakini Yoshua alibaki nje (Kut 24:13). Vile vile Yoshua hakutoka katika hema ambamo Musa alikutana na Mungu (Kutoka 33:11; Hesabu 11:28). Siku moja, Waisraeli walipomwasi Mungu jangwani, Yoshua alionyesha imani yake yenye ujasiri ambapo yeye na Kalebu walisimama imara kinyume cha wenzao wote (Hesabu 14:9). Ni yeye aliyewaingiza Waisrael nchi ya ahadi, Kanaani baada ya Musa kupotelea jangwani.

Mtunzi wa tamthiliya hii ya *Nyerere na Safari ya Kanaani* katika Onyesho la Tisa hajamtumia mhusika mtoto Joshua kwa bahati mbaya. Joshua wa kwenye kitabu cha Kutoka ndiye Joshua huyu katika tamthiliya hii. Anatokeza ili kuendeleza safari ambayo baba wa taifa la Tanzania, Mwalimu Nyerere aliianzisha. Mwalimu alikuwa na maono mengi mema juu ya taifa hili toka lipate uhuru, lakini kwa bahati mbaya kabla Tanzania haijafika kwenye ngazi hiyo ya maziwa na asali akatwaliwa na Mola mwaka 1999. Hivyo kwa dhana hii ya mwingilianomatini kuwa matini husemezana na kuhusiana hakika mhimili huu unathibitika wazi. Kuna mwingilianomatini

mkubwa kati ya fasihi na Biblia uliothibishwa na utafiti huu. Tutazame hapa mtoto Joshua anavyotambulishwa azaliwapo;

(___kelele za shangwe; wasanii wanajitupa uwanjani…Naye mtoto Joshua pia anaingia kucheza nao…)

Chanzo: Data za Utafiti katika *Nyerere na Safari ya Kanaani*, (uk.64)

Pia tunaona ndani ya tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello*, Ujenzi na uteuzi wa mhusika mkuu John Okello umefanyika mahsusi. Kuna jambo msanii amekusudia kulifikisha kwa jamii. Kwa hivyo matendo na mazungumzo anayopewa pahala pote alimozungumza na kutenda kumefanyika kwa malengo maalum. Namna John Okello alivyochorwa kumedhihirisha mwingilianomatini wa Biblia katika tamthiliya hii teule ya *Sadaka ya John Okello*. Utendaji wa John Okello na lugha anayopewa unaenda sawia na matendo na mazungumzo ya Mtume Yesu anayezungumzwa katika mapokeo ya Ukristo ndani ya Biblia.

Kwa mfano, katika tamthiliya hii tunaona John Okello amepewa uwezo wa kuona mambo ya rohoni (maono), amepewa uwezo wa kutabiri yatakayotukia baadaye na hakika yakatimia kama alivyosema. Sifa hizi zinaakisi uungu. Kwenye mapokeo ya ukristo ndani ya Biblia, mwenye uwezo wa kuyafanya hayo yote aliyokuwa akiyafanya John Okello kwenye hii tamthiliya ni mtume Yesu tu. Tunaweza kuona sehemu ya maneno anayosema mhusika John Okello kuwa na mwangwi wa Biblia. Anasema;

**JOHN OKELLO**: "…lakini Mungu alinituma nije kuwakomboa ndugu zangu wa visiwani…" (uk 29)

Huu uwezo na uhusika unaendana na mhusika Yesu Kristo katika mapokeo ya Kikristo anayepatikana katika kitabu chao cha Biblia. Hata yeye, Yesu Kristo alidai kuwa ametumwa na Mola wake kuja kumkomboa mwanadamu kutoka kwenye dhambi zake. Muhimili wa mwingilianomatini unathibitika katika kazi hii, ya kwamba kazi yoyote mpya huwa ni zao ama tokeo la matini nyingine tangulizi alizowahi kukutana nazo msanii kabla ya matini hiyo mpya. Kwamba mtunzi anaweza kuvutiwa na mhusika fulani katika matini anayokutana nayo na kutumia matini hiyo akaamua kuzungumza jambo jipya japo kwa kubadilisha jina la mhusika lakini sifa na utendaji wake ukawa uleule aliokutana nao awali katika matini chasili. Kimsingi tumebaini kwamba, katika kazi teule zote tulizotafiti, wahusika wenye mwangwi wa kibiblia wametumiwa. Tunashadidia kwamba kazi hizi ni tokeo la mapokeo ya kikristo aliyokutana nayo mwandishi wa kazi hizi hapo kwanza katika imani yake. Mwangwi huo haujatokea kibubusa. Ipo sababu iliyosababisha utokee na sababu hiyo ni athari ya matini chanzi, Biblia iliyopata kutangulia kabla ya hizi zilizokuja sasa.

### 4.2.4 Nukuu za Biblia

Washadidi wa nadharia ya mwingilianomatini, Bakhtin (1981) na Kristeva (1986) na wenzao wanadai kwamba matini za fasihi huwa zimechota, kunukuu, kugeuza, kuiga kwa namna ya kubeza au kurejelea kwa njia moja au nyingine matini nyingine tangulizi. Kwa hivyo matini uhusiana na kuingiliana kwa namna nyingi tu. Mhimili huu unatupelekea kwenye kuamini kuwa hakuna kazi ya fasihi iliyo halisi yenyewe. Matini mpya lazima ihusiane na matini nyingine zilizotangulia.

Katika tamthiliya hii ya *Nyerere na Safari ya Kanaani* kuna nukuu mbalimbali za Biblia zilizojitokeza ndani ya maonyesho mbalimbali. Matini hizi zinaibua mwangwi kwenye masikio ya msikilizaji, asizisikiapo aiona matini ya Biblia katika kazi husika. Mfano upo katika onyesho la tano (uk 35) ambapo mhusika mkuu Nyerere ananukuu sehemu ya mstari kutoka kwenye Biblia.

**NYERERE**: Shut up! Mfalme Suleiman alisema; Mtoto hupenda mambo ya kijinga moyoni, lakini fimbo ya nidhamu humwondolea ujinga huo…!

(*Nyerere na Safari ya Kanaani*, uk.35)

Maneno haya aliyopewa mhusika huyu yanapatikana katika kitabu cha Biblia. Kitabu kimojawapo alichokiandika Mfalme Suleiman kinaitwa Mithali. Nukuu hiyo aliyoitumia Nyerere ndani ya kazi ya Nyerere na Safari ya Kanaani inapatikana inasema hivi;

> Ujinga umefungwa ndani ya moyo wa mtoto, lakini fimbo ya adhabu itaufukuzia mbali.
>
> Chanzo: Data za Utafiti-*Biblia Takatifu*, (Mithali 22:15)

Sehemu nyingine mtunzi amemchora mhusika wake MARTIN akizungumza kwa kunukuu sehemu ya mstari kutoka kwenye Biblia. Uk wa 49, **MARTIN***:...Mungu amekisikia na kukitakabali kilio cha machozi yako."* Neno kutakabali katika Biblia lina maana ya kukubaliwa na kupokelewa. Lilitumika kwa mara ya kwanza katika kitabu cha Mwanzo 4:4b ambapo watoto wawili wa Adam; Kaini na Habili walienda mbele za Mungu kutoa sadaka, mmoja wao ikakataliwa (Kaini) na mwingine ikatakabaliwa na kupokelewa (Habili) kwa kuwa alitoa sadaka iliyo nzuri ya kupendeza mbele za Mwenyezi Mungu. Nadharia ya mwingilianomatini inaelekeza

kuwa mageuzi yanaweza kufanyika baina ya matini chanzi na matini hii mpya iliyozaliwa. Kuna baadhi ya maneno na tungo zilizotumika zinazobainisha uhusiano uliopo baina ya Biblia na kazi hii ya fasihi. Tumtazame mhusika huyu asemavyo;

**MARTIN***:* ...Vile viboko alivyotuchapa havikutosha hadi turudi Ikulu tena; ili tupomoke na kumsujudia: Kwa jina la Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Nabii Musa anataka, katika madhabahu ile ya ikulu, azighofiri dhambi zetu ili tupate kurithi ufalme wa nchi ya asali na maziwa?

Chanzo: Data za Utafiti katika tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani* (uk.55)

Maneno yaliyotumika katika sehemu hiyo yanahusiana na maneno wayatumiayo viongozi wa makanisa katika kufanya sala ya kuungama na kutangaza msamaha kwa waumini wao wamalizapo kuungama dhambi zao na kutubu mbele ya Mwenyezi Mungu. Wao huanza kutangaza msamaha huo na maneno haya, *"Kwa jina la Baba, na la Mwana na la Roho MTakatifu..."* kwa hivyo mtu asomapo maneno hayo yanayotoka kwenye kinywa cha Martin anaenda kanisani, anaiona hali ya kupiga magoti chini, kusujudu na kuungama dhambi na hatimaye kutangaziwa msamaha na kiongozi wake katika ibada.

Athari ya mapokeo ya kikristo inaonekana waziwazi katika kazi hii kupitia mfano huu. Kwa hivyo upo ubiblia katika tamthiliya hii unaosababishwa na mapokeo ya kiimani aliyokumbana nayo mwandishi wa kazi hii katika maisha yake kabla ya kuandika kazi hii. Pia katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* mtunzi amenukuu na kurejelea baadhi ya mistari na maneno kutoka kwenye Biblia. Kwa hivyo ni kweli

ubiblia umo kwenye kazi hii. Tulimtazama Okello na mazungumzo yake wa wapambanaji wenzake;

**OKELLO**: Usiku wa jana; Mwenyezi Mungu kanionesha katika maono: nyota kubwa. Kimondo kikitokea Tanganyika, kikaseleleka angani na kuzama Zanzibar, ndani ya bahari ya Hindi.

**OKELLO**: Mmesikia? Mbingu zimetulia. Maana yake ni kuwa Field Marshall wa mbinguni, ushindi ametupatia (anaita) Mfaranyaki*!*

Chanzo: Data za utafiti katika *Sadaka ya John Okello* (uk 42)

John Okello amechorwa kama nabii wa mwenyezi Mungu hapa. Mtu mwenye mamlaka, ambaye Mola humjaalia maono akaona mambo yanayotukia katika ulimwengu mwingine. Watu waonao maono ni manabii wa mwenyezi Mungu. Katika Biblia watu hawa wamejitokeza wengi na mara nyingi walitumika pia nyakati za vita katika masimulizi mbalimbali ndani ya Biblia. Manabii hawa hutangulia mbele na kusema na watu mambo yatakayojiri kuhusu vita au tukio hilo lililo mbele ya jamii kwa wakati huo.

Katika Biblia kuna kijana aitwaye Samweli. Kijana huyu alikuwa mcha Mungu na alikuwa akitumika chini ya Mzee mmoja aitwaye Eli. Siku moja awapo usingizini alionyeshwa maono kuhusu bwana wake, Mzee Eli. Alipoyaona maono hayo kesho yake alimwambia mzee wake juu ya yote aliyoonyeshwa na mwenyezi Mungu kumuhusu mzee huyo, na kitu ambacho mzee huyo alipaswa kufanya kutokana na maagizo ya mwenyezi mungu ambayo kijana huyu aliyaona. Biblia inasema,

> Naye Samweli akalala hata asubuhi, akafungua milango ya nyumba ya Bwana. Samweli akaogopa kumjulisha Eli maono hayo.

Chanzo: Data za Utafiti katika Biblia Takatifu 1 Samweli 3:15.

Katika kisa hiki, kijana huyu mcha Mungu anaonyeshwa maono kuhusu familia ya kiongozi wake wa kanisa. Mambo yatakayotukia na ghadhabu ambayo mwenyezi Mungu ameipata kutokana na vijana wa mzee huyu, Mzee Eli kutenda dhambi. Utafiti ulibaini namna nukuu hizi zilivyogeuzwa ama kubadilishwa lakini zikirejea dhana ile ile ya msingi, uungu na uonaji wa maono kuhusu matukio yatakayotukia hapo mbele. Mahala pengine mhusika mkuu John Okello amesema maneno haya, “Kazi aliyonituma baba imekamilika.” Uk.56 (Sadaka ya John Okello). Matini hii inatoa mwangwi wa maneno ya Yesu akiwa msalabani amalizapo kazi ya kumkomboa mwanadamu kama inavyoelezwa kwenye Biblia. Biblia imeandika hivi;

> *Baada ya hayo Yesu, hali akijua ya kuwa yote yamekwisha kumalizika ili andiko litimizwe, akasema, naona kiu…alipokwisha kuipokea ile siki akasema, Imekwisha. Akainama kichwa, akasalimu roho yake.*
> (Yohana 19: 28-30).

Nukuu hizo kwa mujibu wa utafiti huu zinaakisi mwangwi wa Biblia katika tamthiliya hii ya *Sadaka ya John Okello*. Kwa hivyo ni ukweli bayana kuwa upo mwangwi wa Biblia katika matini hii. Mhimili wa nadharia hii ya mwingilianomatini kuwa kazi moja hunukuu ama kugeuza baadhi ya vipengele katika kuzaa ama kuunda matini mpya ni sahihi na umethibitika katika kazi hii kama tulivyoubanisha.

Kimsingi nadharia ya mwingilianomatini inadai kuwa matini za fasihi huwa zinanukuu, kugeuza au kurejelea kwa njia moja au nyingine matini nyingine tangulizi. Kwa hivyo matini huhusiana na kuingiliana kwa namna mbalimbali. Kutokea kwa nukuu za kibiblia katika tamthiliya hizi mbili teule kunathibitisha dai la wanazuoni hawa. Kuna pengo la karne nyingi sana tangu kuandikwa kwa Biblia na kazi hizi za Emmanuel Mbogo. Lakini zinaposomwa nukuu zake zinaonekana katika

Biblia kwa wasomaji wenye mapokeo ya ukristo. Imethibitika yakini kuwa kazi hizi za Emmanuel Mbogo zinaakisi ubiblia mwingi ndani yake.

### 4.2.5 Matumizi ya Ushairi/Zaburi

Ushairi umetumika pia katika kazi hii ya fasihi tuliyoitafiti. Tutabainisha jinsi ushairi ulivyojitokeza na namna unavyoakisi ubiblia katika kazi hizi za Emmanuel Mbogo. Tunafikiri ni vema kabla ya kusonga mbele tuitazame dhana ya ushairi jinsi ilivyojadiliwa na wataalamu mbalimbali. Baada ya kujadili dhana ya ushairi tutarejea kwenye hoja yetu ya msingi. Massamba, (2003) akimnukuu Shaban Robert, anasema kwamba ushairi ni sanaa ya vina inayopambanuliwa kama nyimbo, mashairi na tenzi na zaidi ya kuwa ni sanaa ya vina ushairi una ufasaha wa maneno machache au muhtasari. Shaaban Robert amezungumza zaidi kuhusu umbo la fani hii katika fasihi. Fafanuzi hii inayotolewa na Shaaban Robert imekaa katika uga wa washairi wa kimapokeo. Kwa mwega aliomo yeye, fasili hii kuhusu dhana ya ushairi ni sahihi.

Mnyampala (1970) anasema kuwa ushairi ni msingi wa maneno ya hekima tangu kale ndicho kitu kilicho bora sana katika maongozi ya dunia kwa kutumia maneno ya mkato na lugha nzito yenye kunata iliyopangwa kwa urari wa mizani na vina maalum. Mwanazuoni huyu anaegemea zaidi katika mkondo wa ushairi wa kimapokeo, ambao kwake msingi mkubwa ni urari wa vina na mizani. Ndilo tunaloliona tunapopitia andiko lake. Maana hii inayotolewa na Mnyapala itatusaidia katika utafiti wetu, hasa tunapozungumza kuhusu dhana ya ushairi. Tutafahamu tunarejelea kitu kipi. Pamoja nao wanazuoni wengine waliojadili dhana hii ya ushairi katika fasihi ya Kiswahili ni Mulokozi na Kahigi (1982:25). Wao wanasema kwamba ushairi ni sanaa inayopambanuliwa kwa mpangilio maalum na fasaha na wenye

muwala, kwa lugha ya picha, sitiari au ishara katika usemi, maandishi au mahadhi ya wimbo ili kuleta wazo au mawazo, kufunza au kueleza tukio au hisia fulani kuhusu maisha au mazingira ya binadamu kwa njia inayogusa moyo. Fafanuzi hii anayoitoa Mulokozi inaeleza dhana za msingi kuuhusu ushairi, katika utafiti huu tunaoufanya tunapata mwanga faafu kuihusu dhana hii. Hivyo basi tunaweza kuhitimisha kwa kusema kuwa ushairi ni kazi ya sanaa yenye kuandikwa au kuimbwa kwa kufuata kanuni za ushairi au kutofuata kanuni za ushairi. Fafanuzi hii inatupeleka kwenye wazo kuwa ushairi waweza kuwa wa kimapokeo yaani unaofuata urali wa vina na mizani au wa kisasa, usiofuata kanuni za urali wa vina na mizani. Jambo lingine la msingi linalosisitizwa katika utungo wa kishairi ni kubeba ujumbe fulani mahsusi.

Tumekwisha kudokeza hapo kwanza kuwa, Biblia ni kitabu kiTakatifu kinachotumiwa na waumini wa dini ya kikristo katika mafundisho ya imani yao. Wanazuoni katika uga wa fasihi wanakubaliana kuwa kitabu hiki ni miongoni mwa mazao makubwa sana ya fasihi ambayo ni vigumu kuchujuka uzuri wake. Metzger na Coogan (1993) wanaelezea Biblia kama kitabu chenye kufasiliwa kama fasihi. Watu wengi wanakubaliana kuhusu thamani ya mafundisho ya fasihi yaliyomo katika Biblia. Ubora wa fasihi ya Biblia umechangiwa na maudhui yake, lugha ya kishairi na ujuzi wa waandishi wake katika kufasiri kazi hiyo. Aina kuu za fasihi zinazojitokeza kwenye Biblia ni nathari na ushairi.

Baadhi ya vitabu katika Biblia vilivyotumia mtindo wa ushairi zaidi ni Zaburi, Mithali, Wimbo Ulio Bora na Ayubu. Bakhtin na Kristeva katika nadharia yao ya mwingilianomatini wanadai kwamba kila usomaji matini huwa ni kijalizo cha msingi cha matini tangulizi na hivyo basi kuigeuza kwa kiwango. Kwa jinsi hii kauli

inayochukuliwa hubadili na kueleza upya kauli asilia kwa kuiambatisha na muktadha mwingine wa kiisimu na kijamii. Hili wanalolisema washadidi wa nadharia hii linadhihirika katika kazi za Emmanuel Mbogo tulizoziteua kutumia katika utafiti huu. Tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani*, imetumia mtindo wa kishairi, ambao umegeuzwa kuendana na muktadha lakini pia ukahusianishwa na mawaidha au maneno ya Mwenyezi Mungu. Kwa sehemu kubwa katika Onyesho la Tisa (Nyerere na Safari ya Kanaani) mtunzi amempa lugha ya kishairi muhusika mkuu NYERERE alipokuwa akiongea na hadhara Ikulu. Tunaposoma beti hizo ubiblia unajitokeza. Baadhi ya beti zenye mwangwi wa Biblia katika masikio ya wasikilizaji na macho ya watazamaji ni hizi:

3. Humu ndani ya mwili, kuna moyo umetulia
Wengine wamwita Roho, udongoni umejikalia
Roho anao uhai, uzima mwili kuugawia
Itajengwa na wenye moyo, hii yetu Tanzania

6. Nakuuliza ewe mwili, ni lipi unaloringia
Ama ni wako ukwasi, na wingi wa zako rupia
Hata Roho akikushauri, ubishi meng’ang’ania
Itajengwa na wenye moyo, hii yetu Tanzania

8. Utaingia hasara, Roho kumpuuzia
Anazo hekima lufufu,aweza kukutunukia
Roho yako ni ‘mungu’, kiungo cha wako Jalia
Itajengwa na wenye moyo, hii yetu Tanzania

Chanzo: Data za Utafiti katika Tamthiliya-*Nyerere na Safari ya Kanaani* (uk.61-64)

Pia tunaposoma tamthiliya ya Sadaka ya John Okello tunakutana na mtindo wa kishairi kutumika. Mtunzi Emmanuel Mbogo ametumia maghani katika kazi yake

hii. Mtindo huu wa kishairi umetumika kwa sehemu sehemu ndani ya kazi hii. Tutazame mfano:

**IDDI**: Field Marshall John Okello!
Mimi shujaa Iddi.
Ninaranda, ninatamba, ninatanda.
Ninatambaa! Ninasambaa.
Mimi Shujaa Iddi, mwana wa Chipoko
Mimi Iddi, mwana wa mamaangu Mwajuma
Mimi niliyekataa kuja duniani
Wakati wangu ulipotimu!
(Onyesho la Tano uk. 22)

Katika onyesho hili, waghani wawili wanajibizana. John Okello na Idd. Mtindo huu ni maarufu sana katika kitabu cha Biblia. Vipo vitabu kabisa (tumevitaja huko juu) ambavyo vimeandikwa kwa mtindo wa kishairi mwanzo hadi mwisho. Baadhi ya hivyo ni *Zaburi* na *Wimbo Uliobora* zilizoimbwa na Mfalme Daudi na Mfalme Suleiman pamoja. Hivi ndivyo ubiblia ulivyodhihirika katika kazi za Emmanuel Mbogo.

Kwa jumla katika sehemu hii tumetazama na kubainisha mwingilianomatini wa Biblia na fasihi katika tamthiliya zetu teule, *Nyerere na Safari ya Kanaani* na *Sadaka ya John Okello*. Tumebainisha na kufafanua ubiblia uliojitokeza kwa kuegema zaidi katika mihimili ya nadharia ya mwingilianomatini iliyoasisiwa na magwiji wawili, Mikhail Bakhtin na Julia Kristeva.

Kuna ubiblia mwingi katika kazi hii ya fasihi na Biblia Takatifu, kitabu kinachotumiwa na wakristo kama tulivyobainisha. Mihimili ya nadharia hii ya mwingilianomatini ndizo sababu zinazoelezwa kuhusu kutokea ubiblia katika kazi

Emmanuel Mbogo. Katika uchambuzi wa data, ubiblia umebainishwa na kuelezwa sababu ya kutokea kwake.

### 4.3 Hitimisho

Katika sura hii ya nne tumejadili mambo mbalimbali. Kwanza tumejadili usuli wa mtunzi wa kazi teule zilizotumika kufanya utafiti huu, Profesa Emmanuel Mbogo. Pili tumejadili mihtasari ya tamthiliya zote mbili, *Nyerere na Safari ya Kanaani* (2015) na *Sadaka ya John Okello* (2015). Tatu tumejadili na kubainisha ubiblia katika tamthiliya zote mbili. Pamoja na hayo tumebainisha pia sababu za kujitokeza kwa ubiblia katika matini hizo. Sura hii ya nne imeonyesha data na kuzichanganua kwa kutumia tamthiliya zilizoteuliwa na Biblia Takatifu ili kuonyesha namna zilivyoingiliana na kuathiriana.

Kimsingi utafiti huu ulibaini kwamba, kuna ubiblia mwingi katika tamthiliya hizi zilizoteuliwa, *Sadaka ya John Okello* na *Nyerere na Safari ya Kanaani*. Ubiblia huo umejitokeza kwa namna mbalimbali. Kwa mfano kwa kuchukua masimulizi baadhi yaliyomo ndani ya Biblia kujenga kisa cha kazi, kutumia nukuu za kibiblia, mitindo ya kibiblia na dhana mbalimbali zilizomo katika Biblia. Mwangwi wa Biblia katika kazi hizi unasikika kwa mtu yeyote aliyepata kukutana na Biblia kabla. Matukio, ujenzi wa visa na mtindo wa mazungumzo ya wahusika unaendana sawasawa na yale yaliyojiri kwenye Biblia kama tulivyobainisha huko juu wakati tukijadili na kubainisha mwangwi wa Biblia katika kazi hizo teule. Mihimili ya nadharia hii ndiyo imetumiwa kueleza sababu za utokeaji wa ubiblia katika kazi hizi za fasihi.

# SURA YA TANO

# 5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Hii ni sura ya mwisho katika tasnifu hii. Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza tumeandika muhtasari kuhusu utafiti na mambo yote ya msingi kuhusu utafiti kwa mfano; tatizo la utafiti, data za utafiti, sampuli na usampulishani n.k. Sehemu ya pili ni hitimisho linalotaja kwa muhtasari matokeo ya utafiti huu uliofanyika wa kuchunguza ubiblia katika kazi teule za Emmanuel Mbogo na hatimaye sehemu ya tatu tumetoa mapendekezo ambayo yalichagizwa na matokeo ya utafiti tulioufanya.

## 5.2 Muhtasari

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuchunguza ubiblia katika kazi teule za Emmanuel Mbogo; *Nyerere na Safari ya Kanaani* (2015) na *Sadaka ya John Okello* (2015) ili kubaini namna mtunzi huyu alivyofumbata ubiblia katika tamthiliya hizo mbili. Utafiti huu ulikuwa na malengo mahsusi mawili ambayo yalijibiwa na maswali mawili. Lengo mahsusi la kwanza lilikuwa kubainisha utokezaji wa ubiblia katika kazi teule za Emmanuel Mbogo, ndani ya tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani* na *Sadaka ya John Okello*. Lengo mahsusi la pili lilikuwa kueleza sababu

za utokezaji wa matini za Biblia katika kazi teule za Emmanuel Mbogo; *Nyerere na Safari ya Kanaani* na *Sadaka ya John Okello*.

Tatizo la utafiti huu limetokana na uelewa wa mtafiti baada ya kupitia vyanzo mbalimbali vya maarifa na kubaini kuwa hakukuwa na utafiti ambao umejikita katika kuchunguza mwingilianomatini wa Biblia katika kazi za mtunzi huyu nguli wa sanaa za maonyesho na filamu hapa nchini Tanzania, Emmanuel Mbogo. Kwa hiyo tatizo la utafiti lilikuwa kuchunguza ubiblia katika tamthiliya za Emmanuel Mbogo, ili kubaini namna mtunzi huyu alivyoifumbata mbinu wa mwingilianomatini kwa kurejelea Biblia katika utunzi wa kazi zake. Kwa kufanya hivyo tumeweza kubainisha mwangwi wa Biblia katika kazi za Emmanuel Mbogo na kueleza sababu za utokezaji wa matini hizo ndani ya kazi teule tulizotumia kufanya utafiti. Utafiti huu ulitazama zaidi tamthiliya mbili za Emmanuel Mbogo; *Nyerere na Safari ya Kanaani* (2015) na *Sadaka ya John Okello* (2015). Utafiti huu umetumia nadharia ya mwingilianomatini katika kuchunguza, kuchambua na kujadili data na matokeo ya utafiti huu.

Katika utafiti huu mbinu za utafiti zinajadiliwa kwa kina katika sura ya tatu. Katika sura hiyo imebainishwa kuwa eneo la utafiti lilikuwa Dar es Salaam. Utafiti huu ulikuwa wa kimaktaba, kwa hiyo Dar es Salaam ilichaguliwa mahsusi kutokana na huduma za maktaba kupatikana kwa uzuri zaidi ikilinganishwa na maeneo mengine hapa nchini Tanzania.  Kazi teule katika utafiti huu zilikuwa tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani* (2015) na *Sadaka ya John Okello* (2015). Kazi hizi mbili ziliteuliwa mahsusi kwa kuonekana kwamba zingewezesha kupatikana kwa data zinazohitajika.

Sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa. Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu kuu moja, mapitio ya maandiko. Mbinu hii ilitusaidia kuchambua tamthiliya zote mbili na kubainisha mwingilianomatini wa Biblia katika tamthiliya hizo. Data za utafiti huu zimechambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo. Utafiti huu umetumia mbinu zisizo za kitakwimu katika kuwasilisha na kujadili data za utafiti. Kwa jumla matokeo ya utafiti huu yametokana na maswali mawili ambayo yalitokana na malengo mahsusi. Kwa hiyo matokeo ya utafiti huu ni kama ifuatavyo; Swali la kwanza lililenga kubaini ubiblia unavyojitokeza katika tamthiliya za Emmanuel Mbogo; tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani* na *Sadaka ya John Okello*. Utafiti huu umebaini kwamba mwandishi ametumia matini za; majina ya kazi (majina ya Biblia), hadithi za Biblia, wahusika wa Biblia, nukuu za Biblia na ushairi wa Biblia katika utunzi wa tamthiliya zake.

Aidha utafiti umebaini kuwa, tamthiliya zote ni matokeo ya mapokeo ya simulizi ya kikristo ambayo mtunzi aliyapata kupitia kitabu cha Biblia kitumiwacho na waumini wa imani hiyo. Katika *Nyerere na Safari ya Kanaani* matini ya safari ya wana wa Israel kutoka utumwani Misri kwenda Kanaani, nchi waliyoahidiwa na Mola wao kwamba watapewa, nchi ya maziwa na asali imetumika kama msingi mkuu katika kuunda kazi hii. Mgogoro kati ya serikali ya Tanzania na wanafunzi wa chuo kikuu kuhusu sera ya kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) wamalizapo masomo yao umetumika kama kioo tu cha kuonyesha namna rais wa kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alivyoanza safari ya kuongoza taifa huru na changamoto mbalimbali alizokutana nazo wakati akiisaidia Tanzania kwenda katika

hatua kubwa kimaendeleo. Rais huyu alitaka nchi yake istawi na kufanikiwa kwa viwango vya juu kabisa, lakini kwa bahati mbaya alifariki kabla ya kuiona nchi yake katika viwango hivyo vya juu vya mafanikio. Mtunzi amemfananisha Mwalimu Nyerere na Nabii Musa, kiongozi wa wana wa Israel safarini kutoka utumwani, pamoja na changamoto nyingi alizokutana nazo njiani naye hakufanikiwa kuingia nchi ya ahadi. Alikufa kabla ya safari kufika mwisho na kuiona nchi ya asali na maziwa. Kwa upande wa tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello*, utafiti huu umebaini kwamba matini ya ukombozi wa mwanadamu alioufanya Mtume Yesu kama inavyoonekana katika kitabu cha waumini wa kikristo, Biblia ndiyo iliyotumika kama msingi wa kuundwa kwa kazi hii. Mtume Yesu aliyatoa maisha yake sadaka, akakubali kufa kwa ajili ya wanadamu. John Okello naye amekubali kufa, alikuwa radhi kupambana na majalibosi yoyote ili mradi tu mwafrika apate uhuru wa kweli. Pamoja na kutambua hatari ilikuwa mbele yake, bado aliendeleza mapambano.

Swali la pili lililenga kueleza sababu za utokezaji wa matini za Biblia katika tamthiliya hizi mbili za mtunzi huyu; *Nyerere na Safari ya Kanaani* na *Sadaka ya John Okello*. Tukirejelea nadharia ya mwingilianomatini yake Julias Kristeva (1980) isemayo kuwa; kazi yoyote ya fasihi ni tokeo la kazi ama matini nyingine zilizopata kuwepo kabla ya hiyo mpya, tulibaini kwamba sababu ya utokezaji wa matini za Biblia katika kazi za Emmanuel Mbogo ni tokeo na athari ya mapokeo ya masimulizi ya kikristo aliyonayo mtunzi wa kazi hizi, Emmanuel Mbogo. Kwa hivyo kazi nyingi alizoandika mtunzi huyu katika miongo ya hivi karibuni zinatoa mwangwi wa Biblia zisomwapo.

Kwa jumla utafiti huu umebaini kwamba tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani* na *Sadaka ya John Okello* zina mwingilianomatini mkubwa wa Biblia. Zisomwapo na watu waliomo katika mkondo sawa na mwandishi mwangwi wa Biblia unasikia masikioni mwao. Sababu kubwa ya utokezaji wa matini hizo ni athari na mapokeo ya ukristo aliyonayo mtunzi Emmanuel Mbogo, aliyoyapata hasa kupitia kitabu kitumiwacho na wakristo katika imani yao, Biblia. Tamthiliya zote hizi mbili zimechanganya vionjo na visa mbalimbali vya Biblia. Emmanuel Mbogo ametunga kazi hizi katika mwaka mmoja (2015), hili linaweza kuchangia katika utunzi wa kazi zenye sifa zinazofanana ndani yake. Utunzi huu umemtaja Emmanuel Mbogo kama mwanamwingilianomatini ambaye anadhihirishwa na utunzi wa kazi zake za fasihi; tamthiliya na riwaya. Ndiyo kusema, mbinu hii ya mwingilianomatini ndiyo inayomtambulisha na kumpa upekee wake na mtindo wake wa utunzi katika uga wa fasihi.

## 5.3 Hitimisho

Utafiti huu unahitimisha kwamba Emmanuel Mbogo anatumia mwingilianomatini katika utunzi wake kwa kuingiza matini za Biblia katika utunzi wa tamthiliya za *Nyerere na Safari ya Kanaani* na *Sadaka ya John Okello*. Katika tamthiliya zote mbili, mtunzi ametumia matini za Biblia ambavyo ni matokeo ya mapokeo ya imani ya kikristo kupitia kitabu chao cha Biblia. Pia iligundulika katika utafiti huu kwamba, mtunzi ameathiriwa na mapokeo ya imani ya kikristo aliyoyapata kupitia Biblia. Masimulizi na mapokeo hayo ndiyo yalitumika kama msingi katika utunzi wa kazi zake hizi tulizozitafiti. Imetokana na mtunzi kuchota malighafi yake kubwa kutunga tamthiliya hizi kutoka katika masimulizi ya kiimani yanayopatikana kwenye

Biblia. Imedhihirika pia kwamba matini yoyote ya fasihi ni tokeo la matini nyingine tangulizi iliyopata kuwepo kabla ya hiyo mpya. Dai hili la nadharia ya mwingilianomatini limethibitishwa katika utafiti huu. Watunzi wa kazi za fasihi huathiriana wao kwa wao. Matini za fasihi husemezana na wakati mwingine hukamilishana kimaana.

## 5.4 Mapendekezo

Utafiti huu umefanywa kwa kupitia tamthiliya mbili za *Nyerere na Safari ya Kanaani* na *Sadaka ya John Okello,* zote zimetungwa na Emmanuel Mbogo. Utafiti huu unapendekeza kwamba tafiti nyingine zinaweza kufanyika katika kazi nyingine za mtunzi huyu ili kuona kama mwingilianomatini huu wa Biblia unaojitokeza katika kazi hizi umejitokeza pia huko.

Emmanuel Mbogo ameandika kazi nyingi; riwaya na tamthiliya, watafiti bado tuna uga mpana wa kutafiti na kung'amua mengi kuhusu kazi hizi. Hii itafaidisha uga wa fasihi kupata vyanzo vingi vya maarifa kuhusu mwingilianomatini katika fasihi ya Kiswahili. Tunaendelea kupendekeza kuwa tafiti zinaweza kufanyika baina ya waandishi wawili tofauti. Tafiti hizo ni muhimu kwani zinaweza kutusaidai upekee wa wandishi na mitindo wanayotumia katika utunzi wa kazi zao.

Pia tunapendekeza kwamba watafiti wengine watazame Uislam unavyojitokeza katika kazi za mtunzi huyu. Zipo tamthiliya zake baadhi ambazo zimegusa jamii za Pwani, kama vile *Sadaka ya John Okello* kisa chake kimechotwa katika nchi ya Zanzibar, bila shaka mwangwi wa Uislam utakuwa umejitokeza humo. Vilevile tamthiliya ya *Malkia Bibi Titi Mohamed, Siti Binti Saad n.k*

**MAREJELEO**

Allen, G. (2000). *Intertextuality*.London: Routledge.

Ambrose, K. N. na wenzake (2015). Mwingilianomatini katika Tamthiliya za Kiswahili: *Mashetani* na *Kijiba cha Moyo*. *Jarida la Swahili Forum*. Dar es Salaam.

Bakhtin, M. M. (1981). *The Dialogic Imagination: Four Essays*. Ed. Michael Holquist. Trans. Caryl Emerson and Michael Holquist. Austin and London: University of Texas Press.

Betorncini, E. (1989). *Outline of Swahili Literature*. Leiden University: Leiden.

Bwelele, E. (2016). Kuchunguza Mtindo katika Tamthiliya za *Sadaka ya John Okello* na *Nyerere na Safari ya Kanaani*. (Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam, Tanzania.

Chama cha Biblia Tanzania. (1997). *Biblia Takatifu*. Dodoma: Chama cha Biblia Tanzania.

Clemence, S.M. (2015). Mbinu za Kitanzia za Kiaristotle katika *Fumo Liyongo* na *Sundiata*. (Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam, Tanzania.

Enon, J. C. (1998). *Educational Research: Statistics and Measurement* ($2^{nd}$ ed). Kampala: Makerere University.

Fadhil, E. (2014). Dhima ya Mtindo katika Tamthiliya za Kihistoria: Utafiti Linganishi wa Tamthiliya ya *Morani* na *Kinjeketile*. (Tasnifu ya Uzamili) Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam, Tanzania.

Herman, L.B. (2015). Dhana ya Mwingilianomatini kwenye Hadithi za Watoto katika Kiswahili. *Kioo cha Lugha*: Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. Dar es Salaam: Dar es Salaam Press.

Jacob, D. M. (2016). Utoaji wa Sadaka ya Fungu la Kumi. Dar es Salaam: Huduma ya Manna.

Kezilahabi, E. (1971). *Rosa Mistika.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Khatib, K. S. (2015). Ufasihi Simulizi katika Riwaya Teule za Shaaban Robert: Mifano kutoka *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad*. (Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam, Tanzania.

Kimambo, S. J. (2015). Matumizi ya Lugha katika *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha*. (Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam, Tanzania.

Kimani, N. (2017). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi. Muhadhara Darasani.* Nairobi: Chuo Kikuu Kenyata.

Kiprotich, J. P. (2013). Mchango wa Mbazi za Biblia katika Ukuzaji wa Fasihi Andishi ya Kiswahili. *Swahili Forum*. Nairobi: University of Oxford.

Kombo, D. K. & Trumph, D. L. A. (2006). *Proposal and Thesis Writing.* Nairobi: Paulines Publications Africa.

Kothari, R. C. (2008). *Research Methodology: Methods and Techniques* (3rd ed). New Delhi: Wishwa Parashan.

Kothari, R. C. (1990). *Research Methodology: Methods and Techniques* (2nd ed). New Delhi: New Age International (P) Ltd.

Kristeva, J. (1980). *Desire in Language: A Semiotic Approach to Literature and Art.* New York: Columbia University Press.

Lema, E.P. (2010). Religion and Fanonist Marxism: The Study of Ngugi's Four Novels. (MA. Literature Thesis). University of Dar es Salaam, Dar es Salaam, Tanzania.

Lemanster, T. (2012), What is Intertextuality. *Great World Text*: A programme of the Centre for Humanities. Wisconsin: University of Wisconsin-Madson.

Macha, N. (2013). Matumizi ya Mtindo wa Mwingilianomatini kwenye Tendi. Makala katika https://onlinetuit.blogspot.com/2017/05/mtindo-wa-mwingilianomatini-kwenye-kazi.html.

Makange, N. (2012). *Sadaka ya Mavuno: Mara Tatu kwa Mwaka*. Dar es Salaam: KKKT-DMP.

Mapara, J (2003). The Bible and Literature: A case study in Shona novels. (M.A Thesis). University of Zimbabwe, Harare, Zimbabwe.

Massamba, D.P.B. (2003). Utunzi wa Ushairi wa Kiswahili. *Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili (III), Fasihi*. Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D. P. B. (2003). Utunzi wa Ushairi wa Kiswahili. *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili (III). Fasihi*. Dar es Salaam: TUKI.

Mbogo, E. (2015). *Nyerere na Safari ya Kanaani*. Dar es Salaam: Karljamer Print Technology.

Mbogo, E. (2015). *Sadaka ya John Okello*. Dar es Salaam: Karljamer Print Technology.

Metzger, K. & Coogan, P. (1993). *The Oxford Companion to the Bible*. New York: OUP.

Mlaga, W. K. (2010). Historia ya Tanzania kuanzia 1960-1980 katika Riwaya Teule za Kiswahili: Uhakiki wa Kihalisia. (Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma, Tanzania.

Mningo, R. A. (2015). Tathimini ya Mwingilianomatini katika Utunzi wa Emmanuel Mbogo: Utafiti Linganishi wa Tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liyongo*. (Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam, Tanzania.

Msacky, E. Y. (2014). Usawiri wa Mwanamke katika *Watoto wa Mama Ntilie*. (Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam, Tanzania.

Msokile, M. (1992), *Misingi ya Hadithi Fupi.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi*:* East African Educational Publisher Ltd.

Mulokozi, M. & Kahigi, K. (1982). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam:T.P.H.

Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mutembei, K. A. (2012). *Korasi katika Fasihi: Nadharia Mpya ya Uhakiki*. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

Ndungo, C. (1993). *Nadharia ya Fasihi Simulizi*. Nairobi: University of Nairobi.

Ngugi, W. T. (1967). *A Grain of Wheat.* London: Heinemann.

Ngugi, W. T. (1982). *The Devil on the Cross.* London: Heinemann.

Njogu, K. & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi:Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K. & Wafula, R. M. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyata Foundation.

Ntarangwi, M. (2004). Uhakiki wa Kazi za Fasihi. (Tasnifu ya Uzamivu). Augustina College, Rock Island, U.S.A.

Plotell, J. P. & Charney, H. K. (1978). *Intertextuality: New Perspectives in Criticism*.New York: New York Literary Forum.

Ponera, A. S. (2014). *Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi*. Dar es Salaam: Karljamer Printing Technology.

Ranji, K. (1999). *Research Methodology: A Step by Step, Guide for Begginers.* New Dehli: SAGE Publication.

Samweli, M. (2013). *Tamthiliya ya Kiswahili:* Kutoka Miviga hadi Filamu. Dar es Salaam: NEVELI Publishers.

Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi.* Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi: Mfululizo wa Lugha na Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTTU

Topan, F. (1974). *Aliyeonja Pepo.* Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

TUKI. (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake.* Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publication Ltd.

Wamitila, K.W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi na Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: Daisy Printers (K) Ltd.

Wanjala, F. S. (2015). Mwingilianotanzu katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika: Mfano wa *Embalu* na *Mwaka Kongwa*. (Tasnifu ya Uzamivu). Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi, Kenya.

Webb, H. (1980). *The African Novel and the Way Forward* in Jones, E (Editor *African Literature Today*. London: Heinemann.